Haliuzwi

MEI 4, 2026

/islamicftz

Dhul-Qadah 17 1447

# IMAAN

ISSN 5618 - NO. 582

Huwatoa watu gizani kwa idhini ya Allah

## Maimam wamuunga mkono Rais kuhusu Tume ya Jaji Chande



# Hoja ya kuhalalisha mirungi yazua mjadala mkali



**Kauli ya Mbunge wa Kondoa Mjini (CCM), Mariam Ditopile, ya kutaka kilimo cha mirungi ihalalishwe imeibua upinzani mkali kila kona, huku Ansaar Muslim Youth Centre (AMYC ikiitaja kuwa hatari kwa mustakabali wa taifa.**

## Rais Dkt. Mwinyi: Ufanisi usimamizi wa Hijja chachu ongezeko la mahujaji Zanzibar




Rais Mwinyi akizungumza katika hafla ya kuwaaga mahujaji wanaokwenda Makka, Saudi Arabia, iliyofanyika Msikiti wa Jamiu Zinjibar

**Mwinyi afungua milango ya uwekezaji kwa wafanyabiashara wa Uturuki**

Nini kitafuata baada ya UAE kujitoa OPEC?

## Hatari za kudai umiliki wa msikiti uliowekwa Wakfu



## Sheikh Ibrahim Twaha: Elimu na maadili msingi wa mafanikio ya vijana



## Viongozi wa Kiislamu wataka miongozo ya kimaadili ya AI



Mdhamini wa Taasisi ya Awqaf Tanzania ambaye pia ni Mwenyekiti wa Taasisi ya The Islamic Foundation (TIF), Aref Nahdi

# FIQH YA WAKFU WA MSIKITI: Umuhimu, vigezo na hukmu zake

**Katika maisha ya Kiislamu, masuala ya mali na ustawi wa jamii yanachukua nafasi ya kipekee, na miongoni mwa mada muhimu zinazojadiliwa katika Fiqh ni dhana ya Wakf (Waqf).**

**Neno la Kiarabu 'Waqf' lina maana ya kusimamisha au kuzuia. Kisheria, hii ni kutenga mali maalum – ikiwemo ardhi, majengo, au fedha – na kuizuia isiuzwe, isirithiwe, wala kuhamishwa umiliki wake, huku manufaa yake yakielekezwa katika mambo ya kheri.**

**Makala hii inachunguza msingi wa Fiqh unaohusu wakfu wa msikiti, vigezo vyake, na hukmu zake kulingana na mafunzo ya Kiislamu.**

## Fadhila endelevu na thawabu za kudumu

Wakfu wa msikiti una nafasi ya pekee kwani misikiti ni nyumba za Mwenyezi Mungu na ni kitovu cha ibada. Mwenyezi Mungu anasema katika Qur'an [72:18]: "Na hakika misikiti ni ya Mwenyezi Mungu, basi msiombe pamoja na Mwenyezi Mungu yeyote."

Kujenga msikiti na kuuweka wakfu ni moja ya amali zenye malipo makubwa. Mtume (Allah amshushie rehema na amani) amesema: "Mwenye kujenga msikiti kwa ajili ya Mwenyezi Mungu, Mwenyezi Mungu atamjengea nyumba katika Pepo." [Bukhari na Muslim].

Zaidi ya hayo, wakfu huu huwa ni Sadakat Jariya (sadaka endelevu). Mtume (Allah amshushie rehema na amani) alitaja miongoni mwa vitu vitatu ambavyo huendelea kumletea mtu thawabu hata baada ya kufa kwake ni sadaka endelevu. Hivyo, wakfu wa msikiti unaendelea kumletea thawabu mtoa wakfu kwa muda wote msikiti unapotumika.

## Nguzo za Wakfu (Arkan al-Waqf)

Ili wakfu kuwa halali na sahihi, wanazuoni wa Fiqh wameainisha nguzo kuu nne.

***Mosi,*** Mtoa Wakfu (Al-Waqif): Ili kuwe na wakfu, awali ya yote, lazima awepo mtoaji. Mtoaji ni sharti awe mwenye akili timamu, mwenye umri wa balegh, mwenye hiari (asiye na shinikizo), na mwenye kumiliki mali hiyo kisheria.

***Pili,*** Mali ya Wakfu (Al-Mawquf): Ili kuwe na wakfu, lazima iwepo mali inayotolewa huo wakfu. Mali hiyo inapaswa kuwa halali, yenye manufaa yanayotambulika, na iwe inamilikiwa kikamilifu na mtoa wakfu wakati wa kuitoa.

***Tatu,*** Mnufaika (Al-Mawquf 'Alayh): Nguzo ya tatu ni mnufaika/wanufaika. Kwa wakfu wa msikiti, wanufaika ni Waislamu wote. Hii inajulikana kama Waqf Khayri (wakfu wa kheri kwa umma).

***Nne,*** Sigha (Tamko au Nia): Hii Ni ile kauli au kitendo kinachoonesha nia ya wakfu, kama vile kusema: "Nimeweka wakfu jengo hili kuwa msikiti." Ni bora tamko hili liandikwe na kuwe na mashahidi.

## Vigezo maalum na hukmu za kisheria

Kuna kanuni muhimu zinazozingatia utunzaji na matumizi ya wakfu wa msikiti. Kanuni ya kwanza ni kudumu kwa mali, yaani mali ya wakfu lazima iwe ya kudumu kama vile ardhi au jengo.

Kadhalika, kuwe na uhuru wa umma, ikimaanisha, msikiti unapotolewa kuwa mali ya

# FIQH YA WAKFU WA MSIKITI:
# Umuhimu, vigezo na hukmu zake

umma wa Waislamu, haifai kuwa mali binafsi tena. Tukumbuke kanuni ya wakfu kuwa unapothibiti, hauuzwi, haurithiwi, haugawiwi kwa mtu au kikundi kama zawadi, wala hauwekwi rehani.

Asili ya haya ni hadith iliyosimuliwa na Umar Ibn al-Khattab (Allah amridhie) ambapo Mtume (Allah amshushie rehema na amani) alimwagiza: "Shikilia asili yake, na utoe sadaka kwa matunda yake." Hii ina maana kuwa mali yenyewe hubaki, ila manufaa yake ndiyo hutumika.

## Hatari za kudai umiliki na maslahi binafsi ya msikiti

Moja ya changamoto zinazokabili wakfu Tanzania ni jaribio la kurithi au kudai umiliki wa msikiti, jambo ambalo ni kinyume cha Sharia, ni kula mali isiyo halali na ni dhambi kubwa kwa familia au wasimamizi.

Mwenyezi Mungu anatahadharisha katika Qur'an [2:188]: "Wala msile mali zenu baina yenu kwa batili..." Familia ya aliyeanzisha wakfu haina haki ya kuurithi, hata hivyo wanaweza kupewa usimamizi ikiwa wana uadilifu na watatimiza wajibu wao bila ya kutumia msikiti kwa maslahi binafsi.

Kudai umiliki wa msikiti au kujimilikisha mali ya wakf ni jambo lenye hatari kubwa sana kiimani, kisheria na kijamii. Katika Fiqh ya Kiislamu, kitendo hicho sio tu ni "batili" bali ni chanzo cha dhambi kubwa na adhabu nzito.

## Hatari za kudai umiliki wa wakfu

Hatari zinazojitokeza kwa mtu au jamii inapodai umiliki wa msikiti bila haki ni nyingi. Hapa tutataja baadhi.

Mosi, hatari kubwa zaidi ni kiroho na kiimani. Mtu anapodai mali ya Mwenyezi Mungu, anajihusisha na dhambi ya "Ghulul" (khiyana). Qur'an inasema "Na atakayefanya khiyana, atayaleta Siku ya Kiyama aliyoyafanyia khiyana, kisha kila mtu atalipwa kwa aliyo yachuma, kwa ukamilifu; wala hawatadhulumiwa." [Qur'an, 3:161].

Hatari ya pili na ambayo pia dhambi kubwa ni ubadhirifu wa mali ya umma au kujichukulia ngawira kabla haijagawanywa kihalali. Hatari ya tatu ni kula mali ya haramu na wizi wa mali ya Allah Aliyetukuka. Mtoaji wakfu (Mwuqif) amekusudia kummilikisha Mwenyezi Mungu, na hivyo kudai umiliki wake ni sawa na kuiba mali ya Mungu. Qur'an inaonya vikali: "Wala msile mali zenu baina yenu kwa batili..." [Qur'an, 2:188]. Kwa msingi huo, mapato yoyote ya haramu anayoyapata mtu kutoka katika msikiti huo, (kama kupangisha sehemu zisizo halali), yanamletea laana badala ya baraka.

Hatari ya nne ni kupoteza Ikhlas (Ukweli wa Nia). Wakfu unahesabika kama Sadaka Jariya. Hivyo, ikiwa mrithi au mdai atakuwa anamiliki mali hiyo binafsi, anakuwa anavunja fungamano na Mwenyezi Mungu na kufanya ibada hiyo kuwa batili mbele Yake.

Hatari ya tano ni kwamba, kisharia, katika hukmu za Wakfu, msikiti unaangukia kwenye kundi la "mali ya Mwenyezi Mungu" au mali ya umma. Kwa kukiuka kanuni kuu ya wakfu ya mali kutoruhusiwa kuuzwa, kurithiwa, kutolewa zawadi au kuwekwa rehani; kudai huko umiliki ni kukanusha msingi huu.

Hadith ya Umar ibn al-Khattab inasema: "Shikilia asili yake...". Kudai umiliki ni jaribio la kufuta amri hii ya Mtume (Allah amshushie rehema na amani), jambo ambalo nalo ni hatari kubwa pia.

Hakuna mtu anayeweza kurithi msikiti. Ikiwa familia inajaribu kuurithi, wanafanya dhambi kubwa. Mamlaka ya kisheria (kadhi au mahakama) inaweza kubatilisha madai yao na kuwatoa kwa nguvu, na wakati mwingine wanaweza kushtakiwa kwa ufisadi au wizi.

Kuna hatari ya sita, ya kijamii, nayo ni kuwanyima Waislamu Haki yao. Msikiti ni mali ya umma wa Waumini. Mtu anapoudai, anazuia Waislamu wengine kutumia haki yao ya ibada na manufaa ya wakfu. Hii inaweza kusababisha migogoro, chuki, na mgawanyiko katika jamii.

Pengine sababu inayopelekea haya ni kutafuta kutumia mapato ya msikiti kwa maslahi binafsi badala ya kuyatumia kwa matengenezo, mishahara ya imamu, au misaada ya maskini, jambo ambalo husababisha msikiti kudhoofika na kuharibika.

Hatari kubwa zaidi ni Siku ya Kiyama ambapo Mtume (Allah amshushie rehema na amani) ametoa onyo la kutisha kuhusu wale wanaorithisha au kubadilisha mali za wakfu. Madai ya uongo ya umiliki wa mali iliyowekwa kwa ajili ya Mungu inaweza kumsababishia mtu hasara kubwa siku ya Kiyama kwa kuwa mtu huyo anakuwa amefanya khiyana.

## Je, ni halali kuuza msikiti?

Kwa kanuni ya msingi, ni haramu kuuza mali ya wakfu. Hata hivyo, wanazuoni kama Ibn Qudamah katika kitabu chake Al-Mughni wameruhusu kuuza wakfu wa msikiti ikiwa kuna dharura kali, kama vile msikiti kuharibika kabisa na kuwa haufai tena kwa ibada, na kwa sharti kwamba fedha zitapatikazo zitatumika kujenga msikiti mwingine.

## Hitimisho

Wakfu wa msikiti ni msingi mkubwa wa ustawi wa jamii ya Kiislamu. Unahakikisha uwepo wa nyumba za ibada na kuendeleza kheri kwa vizazi vijavyo.

Hivyo, ni wajibu wa Waislamu wote, na hasa wasimamizi wa wakfu, kuzingatia hukmu hizi za Fiqh ili kulinda mali hiyo na kuhakikisha baraka zake zinadumu.

Kuelewa sheria hizi kunasaidia kulinda mali ya wakfu, kuepuka migogoro, na kuhakikisha manufaa yanaelekezwa katika maagizo ya Mwenyezi Mungu. Tanbihi za hatari kadhaa za kujimilikisha waqfu ya mskiti zizingatiwe.

***Imetayarishwa na Idara ya Elimu ya Awqaf Tanzania***



NA MWANDISHI WETU

# Kampuni 3 zakidhi vigezo halal DSE robo ya kwanza 2026

**■ Kwa mujibu wa ripoti hiyo , kampuni zilizokidhi vigezo vya halal ni Swissport Tanzania, Twiga Cement (TPCC) na TOL Gases, huku Vodacom Tanzania ikitajwa kuwa si halal kabisa.**

Ni kampuni tatu tu kati ya takribani 28 zilizoorodheshwa katika Soko la Hisa la Dar es Salaam (DSE) zilizokidhi vigezo vya halal kwa mujibu wa ripoti mpya ya kampuni ya Shirkah ya robo ya kwanza ya mwaka 2026.

Kwa mujibu wa ripoti hiyo , kampuni zilizokidhi vigezo vya halal ni Swissport Tanzania, Twiga Cement (TPCC) na TOL Gases, huku Vodacom Tanzania ikitajwa kuwa si halal kabisa.

Ripoti hiyo inaeleza kuwa kwa kampuni zilizokidhi vigezo, wawekezaji wanashauriwa kununua au kushikilia hisa, wakati kwa zile zisizokidhi, hatua za kuuza na kufanya utakaso wa mapato zinapendekezwa. Hata hivyo, licha ya TOL kukidhi vigezo vya halal, ripoti hiyo imeweka kampuni hiyo katika kundi la tahadhari kwa vigezo vya kiuwekezaji.

Kwa upande wa utendaji wa soko, fahirisi ya halal ya Shirkah imeonyesha kuimarika, ikikua kwa asilimia 19.02 katika robo hiyo, ikiwa na mtaji wa soko wa takribani Sh trilioni 1.447.

Twiga Cement iliongoza kwa ongezeko la asilimia 20.33, ikifuatiwa na Swissport kwa asilimia 19.31, wakati TOL Gases ilishuka kwa asilimia 12.75.

Kwa muktadha huo, ripoti ya Shirkah inaonyesha kuwa licha ya maendeleo hayo, idadi ya kampuni zinazokidhi vigezo vya uwekezaji wa halal katika DSE bado ni ndogo, jambo linalowahitaji wawekezaji kufanya uchambuzi wa kina kabla ya kuwekeza.

Katika maendeleo ya robo hiyo, Shirkah ilizindua kampeni ya "Shirkah Mtaani" inayolenga kutoa elimu ya uwekezaji moja kwa moja kwa wananchi, pamoja na kuimarisha huduma ya "Shirkah Nunua" ya kurahisisha biashara ya sukuk katika DSE.

Kupitia programu yake ya kidijitali ijulikanayo kama Shirkah Invest (Shirkah Wekeza), hivi sasa, wawekezaji wanapata fursa ya kuwekeza katika KCB Mapato Sukuk iliyoziduliwa mwezi uliopita. Pia Shirkah ilianzisha "Na'di Shirkah", klabu ya uwekezaji inayowawezesha watu wenye mitaji midogo kushiriki katika uwekezaji mkubwa.

Shirkah ni kampuni inayojihusisha na uwekezaji unaozingatia misingi ya halal katika maeneo mbalimbali kama hisa, sukuk, mifuko ya uwekezaji, mali zisizohamishika na biashara ndogo ndani na nje ya nchi, hasa katika ukanda wa Afrika Mashariki na Kusini mwa Afrika (SADC)

Wakati huohuo, ripoti nyingine iliyotolewa na Siraat Shariah Audit and Advisory imeonyesha kuwa bidhaa ya sukuk zimeendelea kuwa na ushindani mkubwa, zikitoa mapato ya kati ya asilimia 10.5 hadi 12 kwa mwaka, hali inayoonyesha kuwa uwekezaji unaozingatia Sharia unaweza kuwa mbadala wenye tija ukilinganisha na njia za kawaida za kuweka fedha benki.

Kwa mfano, KCB Mapato Sukuk ambayo kwa sasa iko katika awamu ya ununuaji, wawekezaji watapata faida ya asilimia 11 kwa mwaka baada ya zoezi la uuzaji wa awali (IPO subscription), CRDB Al Barakah Sukuk inalipa asilimia 12 kwa mwaka, huku Sukuk ya Serikali ya Zanzibar ikitoa asilimia 10.5 kwa mwaka, kwa mujibu wa ripoti hiyo.

Hali hiyo inaonyesha kuwa uwekezaji unaozingatia Sharia unaweza kuwa mbadala wenye tija ukilinganisha na njia za kawaida za kuweka fedha benki, ambazo kwa kipindi hicho zilitoa faida ya chini zaidi.

## Taswira ya fedha za Kiislamu Tanzania

Kwa ujumla, sekta ya fedha za Kiislamu nchini bado iko katika hatua ya ukuaji. Tanzania ina takribani benki tano za Kiislamu au madirisha yake, zinazochukua karibu asilimia 5 ya sekta ya benki, pamoja na waendeshaji watatu wa takaful na mifuko miwili ya uwekezaji wa halal.

Katika soko la mitaji, kuna zaidi ya sukuk 10 za kampuni binafsi, pamoja na baadhi zilizoorodheshwa hadharani, hali inayoonyesha ukuaji wa taratibu wa bidhaa za kifedha zinazozingatia Sharia.



ذوالقعدة

HABARI
DAR ES SALAAM

NA MWANDISHI WETU

# Rais Mwinyi: Ufanisi usimamizi wa Hijja chachu ongezeko la mahujaji Zanzibar



Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Alhaj Dkt. Hussein Ali Mwinyi, amesema Zanzibar imeendelea kupata mafanikio katika usimamizi wa Hijja kila mwaka, hali inayochangia kuongezeka kwa idadi ya mahujaji.

Aidha, Rais Mwinyi ameahidi kuwa Serikali kupitia Kamisheni ya Wakfu na Mali ya Amana itaendelea kuimarisha huduma za Hijja na kushughulikia changamoto zinazowakabili mahujaji.

Rais Mwinyi alitoa kauli hizo katika hafla ya kuwaaga mahujaji wanaokwenda Makka, Saudi Arabia, iliyofanyika Msikiti wa Jamiu Zinjibar, Kiembe Samaki, Mkoa wa Mjini Magharibi.

Hata hivyo, Mwinyi alikiri kuwa mafanikio haya yasingepatikana bila ushirikiano wa wadau wakiwemo Kamisheni ya Wakfu na Mali ya Amana, Umoja wa Taasisi za Hijja Zanzibar na wengine.

Mwinyi, zaidi ya hayo, alisifu ushirikiano wa wadau hao katika kufanikisha safari za Hijja.

Rais Dkt. Mwinyi, katika hotuba yake, alisisitiza umuhimu wa ibada ya Hijja kama Nguzo ya Tano ya Uislamu na kuwataka mahujaji kudumisha nidhamu na mwenendo mwema.

Halikadhalika, aliishukuru Serikali ya Saudi Arabia, taasisi zinazohudumia Hijja, Shirika la Ndege la Saudi Arabia pamoja na Ubalozi wa Tanzania kwa mchango wao katika kuhakikisha huduma bora kwa mahujaji wa Zanzibar.

Rais Dkt. Mwinyi aliongeza kuwa Serikali inaendelea kukamilisha hatua za kisheria kuimarisha Mfuko wa Hijja wa Zanzibar ili kuongeza fursa kwa wananchi wengi zaidi kushiriki ibada hiyo.



NA MWANDISHI WETU

# Mwinyi afungua milango ya uwekezaji kwa wafanyabiashara wa Uturuki

## Kwa upande wake, Balozi Isikci ameihakikishia Zanzibar kuendelea kushirikiana na Tanzania katika mchakato wa kufanikisha maendeleo ya kiuchumi


Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Dkt. Hussein Ali Mwinyi, amezikaribisha kampuni na wawekezaji kutoka Uturuki kuwekeza nchini, hususan katika sekta za biashara, nishati na miundombinu.

Dkt. Mwinyi alitoa wito huo Mei 2, 2026, alipokutana na Mkurugenzi Mkuu anayeshughulikia masuala ya Afrika kutoka Wizara ya Mambo ya Nje ya Uturuki, Balozi Volkan Isikci, aliyefika Ikulu Zanzibar akiongozana na Balozi wa Uturuki nchini Tanzania, Balozi Bekir Geze.

Dkt. Mwinyi alisema hatua hiyo itasaidia kuimarisha uhusiano wa kihistoria kati ya nchi hizo mbili na kufungua fursa mpya za ushirikiano katika biashara na uwekezaji.

Aidha, alisisitiza umuhimu wa wawekezaji kuwekeza katika sekta za kimkakati zikiwemo nishati, kilimo, utalii, afya na miundombinu, pamoja na kuongeza thamani ya mazao ya ndani.

Kwa upande wake, Balozi Isikci ameihakikishia Zanzibar kuendelea kushirikiana na Tanzania katika mchakato wa kufanikisha maendeleo ya kiuchumi kupitia sekta mbalimbali, ikiwemo elimu, afya, kilimo na utalii.



DAR ES SALAAM

NA YUSUPH AMIN

# Maimam wamuunga mkono Rais kuhusu Tume ya Jaji Chande



## Wagusia maridhiano kitaifa, suluhu

Umoja wa Maimam Tanzania (UMATA) umetoa msimamo wake kuhusu maridhiano ya kitaifa kufuatia kuwasilishwa kwa Ripoti ya Tume ya Kuchunguza Matukio ya Uvunjifu wa Amani wakati na baada ya Uchaguzi Mkuu wa Oktoba 29, 2026, ukisisitiza kuwa maridhiano ni msingi wa kuponya Taifa.

Msimamo huo ulitangazwa Jumatano, Aprili 29, 2026 na Mwenyekiti wa Baraza la Maimam na viongozi wa Kiislamu Tanzania, Sheikh Mussa Kundecha alipokuwa akisoma tamko la umoja huo mbele ya waandishi wa habari jijini Dar es Salaam.

Sheikh Kundecha alisema kikao cha umoja huo kimechambua na kutathmini kwa kina ripoti hiyo na kutoa mapendekezo ya namna ya kufanikisha maridhiano yatakayorejesha utulivu na mshikamano nchini.

Katika tamko hilo, Sheikh Kundecha alisisitiza umuhimu wa maridhiano jumuishi yatakayozingatia haki, ukweli na uadilifu, akieleza kuwa maridhiano si hiari bali ni amri ya dini.

Alisema UMATA inampongeza Rais Samia kwa ujasiri wa kuunda Tume huru yenye wataalamu wanaotambulika ndani na nje ya nchi katika masuala ya sheria, diplomasia, ulinzi, intelijensia na upelelezi.

Pongezi hizo zinatokana na kauli ya Rais iliyojaa hisia kali za kusikitishwa na matukio ya Oktoba 29, 2025, pamoja na ahadi yake ya kuunda Tume Huru ya Jinai kwa ajili ya kuchunguza waliochochea ghasia wakati na baada ya uchaguzi.

Akitoa mapendekezo ya suluhisho la muda mrefu, Sheikh Kundecha alishauri kuwepo kwa maridhiano ya kitaifa yatakayogusa malalamiko na maumivu ya jamii zote za Watanzania.

Hata hivyo, alisisitiza kuwa maridhiano hayo lazima yahusishe madai ya ubaguzi katika ajira na fursa, ubaguzi wa kidini na kikabila, akieleza kuwepo kwa malalamiko kuhusu watu wa dini au kabila moja kutawala baadhi ya idara nyeti za serikali ilihali nchi ina Watanzania wa dini na makabila tofauti.

"Maridhiano pia yaangalie mambo yanayolaumiwa sana katika mwenendo wa kesi zinazohusu ugaidi na uhaini.

"Yapo malalamiko makubwa kwa upande mmoja wa dini kuhusu viongozi wao wengi kukamatwa kwa tuhuma za ugaidi na kukaa jela kwa zaidi ya miaka 10 bila kuhukumiwa; wengine hawapelekwi mahakamani, kesi haziendelei, wengine wamefia jela, na wengine wamekamatwa familia nzima bila kujulikana makosa yao...," alisema Sheikh Kundecha na kuonya kuwa hali hiyo ikiendelea inaweza kusababisha matatizo siku zijazo.

Aidha, alisisitiza umuhimu wa serikali kuharakisha mchakato wa kuunda Tume ya Jinai yenye mamlaka ya kisheria kuchunguza, kushtaki na kuhakikisha wahusika wote wanachukuliwa hatua bila kuonewa haya, kuangalia cheo au nguvu za kisiasa.

Akizungumza katika tukio hilo, Amir wa UMATA, Imam Suleiman Abdallah aliwataka wananchi bila kujali itikadi zao kuthamini na kulinda amani ya nchi.

Alisema kwa miaka mingi Watanzania wameishi kama ndugu bila kubaguana kwa misingi ya dini, akisisitiza kuwa Uislamu unahimiza maridhiano na upendo miongoni mwa waumini na jamii kwa ujumla.

Aidha, aliwataka Masheikh, maimam na viongozi wa dini kuendelea kuhubiri amani na kudumisha mshikamano wa kitaifa.

Kwa upande wake, Katibu Mkuu wa Jumuiya ya Almallid, Sheikh Rajab Katimba aliwakosoa wanaopinga ripoti ya Tume ya Rais ya Kuchunguza Matukio ya Uvunjifu wa Amani wakati na baada ya Uchaguzi Mkuu wa Oktoba 29.

Alisema hatua ya Rais kuanzisha tume hiyo ni sehemu ya juhudi za kudumisha amani, utulivu na umoja, kwani ni miongoni mwa vipaumbele muhimu vya taifa.

NA MWANDISHI WETU

# Sheikh Ibrahim Twaha: Elimu iambatane na maadili



**Sheikh Twaha aliyasema hayo katika mhadhara maalum ulioandaliwa na Shule ya Sekondari Forest Hill na kuhudhuriwa na wanafunzi, walimu na wazazi, ambapo alisisitiza umuhimu wa elimu kuambatana na malezi bora ya kiroho.**

Mhadhiri maarufu na Imam wa Masjid Haqq uliopo mjini Morogoro, Sheikh Ibrahim Twaha amesema mafanikio ya mwanafunzi hayapimwi tu kwa ufaulu darasani bali pia kwa mwenendo wake katika jamii.

Sheikh Twaha aliyasema hayo katika mhadhara maalum ulioandaliwa na Shule ya Sekondari Forest Hill na kuhudhuriwa na wanafunzi, walimu na wazazi, ambapo alisisitiza umuhimu wa elimu kuambatana na malezi bora ya kiroho.

Sheikh Twaha, ambaye pia ni Mkurugenzi Mtendaji wa taasisi ya The Islamic Foundation, alisema vijana wanapaswa kujitambua mapema, kuweka malengo ya maisha na kuepuka vishawishi vinavyoweza kuharibu mustakabali wao, ikiwemo matumizi ya dawa za kulevya, uvivu na tabia zisizofaa.

Aliongeza kuwa nidhamu, uwajibikaji na heshima kwa walimu ni mambo muhimu yatakayowawezesha wanafunzi kufanikiwa si tu kitaaluma bali pia katika maisha ya kijamii.

Muhadhara huo ulilenga kuwajengea vijana misingi imara ya maadili na kuwahamasisha kuthamini muda pamoja na kushikamana na maadili ya dini ili kuwa raia wema wenye mchango chanya kwa taifa.

Kwa upande wake, uongozi wa Shule ya Sekondari Forest Hill ulisema kuandaa mihadhara ya aina hiyo ni sehemu ya mkakati wa kutoa elimu jumuishi inayojumuisha taaluma na maadili, na utaendelea kushirikiana na taasisi mbalimbali kuwajengea wanafunzi msingi thabiti wa maisha.

Baadhi ya wanafunzi waliohudhuria mhadhara huo walieleza kufurahishwa na mafunzo waliyoyapata, wakisema yamewapa mwanga wa namna ya kuishi kwa nidhamu na kujiandaa vyema kwa maisha ya baadaye.

Mhadhara huu ni sehemu ya muendelezo wa mihadhara ambayo taasisi ya The Islamic Foundation, chini ya Mwenyekiti Aref Mbaraka Nahdi, imekuwa ikiandaa kwa ajili ya kulingania, kutoa elimu ya dini na maadili kwa makundi mbalimbali na Waislamu kwa ujumla.

# MATUKIO KATIKA PICHA

Na abdulrahman Omar
0655 763 580



## Mhadhara maalum ulioandaliwa na Shule ya Sekondari Forest Hill na kuhudhuriwa na wanafunzi, walimu na wazazi







**HABARI**
**DODOMA**

NA MWANDISHI WETU

# Mbunge aliyetaka mirungi ihalalishwe apingwa kila kona

Kauli ya Mbunge wa Kondoa Mjini (CCM), Mariam Ditopile ya kuitaka Serikali kuhalalisha zao la mirungi imezua upinzani mkali, ikiwemo kutoka kwa Ansaar Muslim Youth Centre (AMYC) waliotaja wazo kama “hatari kwa mustakabali wa taifa.”

Mbunge Ditopile alitoa pendekezo hilo Aprili 29, 2026 bungeni wakati akichangia hotuba ya bajeti ya wizara ya kilimo, akidai mirungi inaweza kuongeza mapato ya taifa na kuwasaidia wakulima, huku akihoji msingi wa kisheria ulioifanya iwekwe katika kundi la dawa za kulevya.

Hata hivyo, AMYC wamesema hoja hiyo “si tu dhaifu kitaalamu, bali ni hatari kwa mustakabali wa taifa,” wakisisitiza kuwa kuhalalisha mirungi kunapingana moja kwa moja na Sheria ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya ya mwaka 2015.

Katika tamko lao refu na la kina kupinga hoja hiyo, AMYC wamesema “kuhalalisha mirungi kutasababisha kudhoofisha mamlaka ya sheria, kudharau juhudi za kitaifa za kupambana na dawa za kulevya, na kufungua mlango wa uhalifu na mmomonyoko wa maadili.”

Kuhusu hoja ya mapato, AMYC wameeleza kuwa ni “upotoshaji mkubwa” kudai mirungi inaweza kuleta maendeleo, wakionya kuwa faida za muda mfupi haziwezi kufidia madhara ya muda mrefu kama gharama za matibabu ya uraibu, kupungua kwa nguvu kazi, pamoja na kuongezeka kwa umaskini na uhalifu.”

Aidha, wamekumbusha wajibu wa Serikali kulinda ustawi wa wananchi: “Serikali ina wajibu wa kulinda afya na maadili ya jamii, si kukusanya mapato kwa gharama ya maisha ya wananchi.”

Wameongeza kuwa mirungi “hulewesha akili, husababisha utegemezi na hupunguza tija,” hivyo kuhalalishwa kwake ni “sawa na kuhalalisha uharibifu wa kizazi cha vijana.”

Kwa mtazamo wa kidini, taasisi hiyo imenukuu hadithi ya Mtume (rehema na amani zimshukie): “Kila kinacholewesha ni haramu,” na kufafanua kuwa wanazuoni wameweka wazi kuwa kila kinachoathiri akili, iwe ni kinywaji au kitu kingine, kinaingia katika hukumu hiyo.



AMYC pia wamegusia maslahi ya umma, wakisema: “Maslahi ya jamii yanapaswa kutangulizwa kuliko faida za kifedha,” wakionya kuwa kuhalalisha mirungi ni “kuweka fedha mbele ya utu wa binadamu.”

Katika ngazi ya kimataifa, wameeleza kuwa hatua hiyo inaweza kuiweka Tanzania katika mgongano na mikataba ya kudhibiti dawa za kulevya, na kuharibu taswira ya nchi.

Kwa msimamo wao wa mwisho, AMYC wamesisitiza: “Kuhalalisha mirungi si sera ya maendeleo — ni sera ya maangamizi,” huku wakiiomba Serikali ikatae pendekezo hilo na kuimarisha mapambano dhidi ya dawa za kulevya.

Kauli hiyo inaongeza uzito wa mjadala unaoendelea nchini kuhusu mustakabali wa zao la mirungi na athari zake kwa jamii.

Ukiacha tamko la AMYC, wadau wengi wametoa maoni mitandaoni kupinga vikali maoni ya mbunge huyo, wakiyataja kama yamepotoka na baadhi wakisema mirungi itaongeza ulevi na kuliingiza taifa katika anguko zaidi la kimaadili.

Mwanamke mmoja, mkazi wa Chanika, anayeishi na mume mtumiaji wa mirungi, ambaye hata hivyo, hakutaka jina lake litajwe amesema maoni ya mbunge, mwanamke mwenzao, yamemshtua mno.

Akifafanua alisema ndoa yake inatetereka kwa sababu ya ulevi wa mumewe wa mirungi na asingependa wanawake wengine wapitie shida anazopitia.

Alisema ukiacha madhara mengi ya kiafya anayopitia mumewe, uraibu umesababisha pesa zote kuishia kwenye matumizi ya mirungi.

Huko Kenya, wadau nao wametoa maoni wengi wakiisikitikia Tanzania kutamani mirungu ihalalishwe ilhali wao nao wanatamani ingeharamishwa nchini kwao.

Watangazaji wa radio maarufu ya 47 Alex Mwakideu na Captain Emmanuel Mwashumbe katika kipindi chao cha asubuhi wameonya Watanzania kuwa mirungi ina madhara mengi na ni bora iendelee kupigwa marufuku.

**MAKALA MAALUM**

**SEHEMU YA 1**

Na Said Rajab
0783 650 803

# Faida 10 za ibada ya Hijja

**Hijja ni nguzo ya tano ya Uislamu, kama alivyoeleza Mtume (rehema na amani zimshukie) aliposema: "Uislamu umejengwa juu ya nguzo tano: Kushuhudia kwamba hapana muabudiwa wa haki ila Allah, na kwamba Muhammad ni mjumbe wa Allah, kusimamisha sala, kutoa zaka, kufunga Ramadhan na kuhiji Makka." [Bukhari].**



# Faida 10 za ibada ya Hijja

Hijja ni nguzo ya tano ya Uislamu, kama alivyoeleza Mtume (rehema na amani zimshukie) aliposema: "Uislamu umejengwa juu ya nguzo tano: Kushuhudia kwamba hapana muabudiwa wa haki ila Allah, na kwamba Muhammad ni mjumbe wa Allah, kusimamisha sala, kutoa zaka, kufunga Ramadhan na kuhiji Makka." [Bukhari].

Hijja imewajibishwa kwa Waislamu wenye akili timamu, waliobalehe na wenye uwezo wa kifedha na kimwili, angalau mara moja katika maisha yao. Allah 'Azza Wajallah' anasema katika Qur'an: "...na kwa ajili ya Mwenyezi Mungu imewajibikia watu wahiji kwenye Nyumba hiyo (Al–Ka'aba), kwa yule awezae njia ya kuendea. Na atakayekanusha basi Mwenyezi Mungu si mhitaji kwa walimwengu." [Qur'an, 3:97].

Makala hii inaangazia faida 10 muhimu ambazo hujaji huzipata wakati na baada ya kutekeleza ibada ya Hijja.

## Kusamehewa madhambi

Mwenye kutekeleza ibada ya Hijja kwa usahihi hupata malipo makubwa mbele ya Allah, ikiwamo kusamehewa madhambi yote yaliyopita. Mtume (rehema na amani zimshukie) amesema: "Umra hadi Umra nyingine ni kafara kati yao, na Hijja iliyokubaliwa (Hajjum Mabrur) haina malipo mengine isipokuwa Pepo." [Bukhari na Muslim].

Hadith nyingine iliyonukuliwa na Muslim inaeleza: "Atakayehiji na akawa hakusema wala kufanya mambo maovu au maasi, atarejea (katika mji wake) kama siku aliyozaliwa na mama yake (yaani bila dhambi yoyote)." Hijja iliyokubaliwa ni ile iliyotekelezwa kwa kufuata muongozo (Sunna) wa Mtume, kwa kutumia mali halali na kuepuka vitendo vyote viovu wakati wa ibada hiyo.

## Kupata Pepo

Hadith zinabainisha wazi kuwa malipo ya milele kwa mwenye kuhiji kwa usahihi ni kuingia Peponi – mahali pa amani, furaha na ustawi wa kudumu. Allah anasema: "Na wale walioamini na wakatenda mema, tutawaingiza katika bustani zipitazo mito chini yake. Watadumu humo milele. Na ahadi ya Mwenyezi Mungu ni ya kweli..." [Qur'an, 4:122].

Aidha: "Mwenye kutenda mema – awe mwanaume au mwanamke, naye akawa ni muumini, hakika tutampa maisha mema, na tutawapa ujira wao kwa mazuri zaidi ya yale waliyokuwa wakiyatenda." [Qur'an, 16:97].

## Kukubaliwa dua

Miongoni mwa fadhila kubwa za Hijja ni kukubaliwa dua. Tukimuomba msamaha Mwenyezi Mungu atajibu dua zetu, kwani yeye hujibu maombi ya waja wake.

Mtume (rehema na amani zimshukie) amesema: "Wale wanaofanya Hijja na Umra ni wageni wa Allah. Wakimuomba atawajibu, na wakimuomba msamaha atawasamehe." [Tirmidhi na Ibn Majah].



## Maisha yenye utulivu

Kwa kuwa Allah husikiliza dua za mahujaji, ni vyema kuomba baraka na mafanikio ya dunia na Akhera. Miongoni mwa nyakati muhimu za kuomba dua ni wakati wa kufanya tawafu kati ya kona ya Yamani na Jiwe Jeusi (Hajar Al–Aswad).

Imepokewa hadith kutoka kwa Abdullahi bin As–Sa'ib (Allah amridhie) kuwa Mtume (rehema na amani zimshukie) alikuwa akisema: "Ewe Allah! Tuletee baraka katika ulimwengu huu na baraka katika ulimwengu ujao, na utulinde na adhabu ya Jehanamu." [Abu Daudi]. Pia imepokewa kuwa malaika 70 huwekwa katika kona ya Yamani na husema "Aamin" kwa dua hiyo. [Tirmidhi na Ibn Majah].

## Jihad kwa wanawake

Kwa wanawake wa Kiislamu, Hijja ni fursa adhimu ya kuchuma thawabu nyingi. Ibada hii huwainua katika daraja ya malipo hadi kufikia hadhi ya Mujahidina (wale wanaopigana katika njia ya Allah).

Mama Aisha (Allah amuwie radhi) alimuuliza Mtume: "Je, hatupaswi kupigana Jihad ilihali tunaona ni amali bora?" Mtume akamjibu: "Jihad bora kwa wanawake ni Hijja iliyokubaliwa (Hajjum Mabrur)." [Bukhari].

## Faida za kiuchumi

Mbali na malipo ya Akhera, Hijja pia huleta manufaa ya kidunia ikiwamo ustawi wa kiuchumi. Waislamu wanaruhusiwa kununua na kuuza bidhaa baada ya kukamilisha ibada zao.


Allah anasema: "Si vibaya kwenu kutafuta fadhila za Mola wenu. Basi mtakapomiminika kutoka Arafa mtajeni Allah kwenye Mash'aril Haram (Muzdalifah) na mkumbukeni yeye kama alivyokuongoeni, ijapokuwa kabla ya hapo mlikuwa miongoni mwa waliopotea." [Qur'an, 2:198].

Pia Allah amesema: "Na utafute kwa aliyokupa Allah makazi ya Akhera. Na wala usisahau fungu lako katika dunia. Na ufanye wema kama Allah alivyokufanyia wema, na wala usitafute kufanya ufisadi katika ardhi. Hakika Allah hawapendi mafisadi." [Qur'an, 28:77].

***Itaendelea katika toleo lijalo, Insha Allah.***

HABARI
MASHARIKI YA KATI

UKHTI FATIMA SS



# Zaidi ya Hijja na Umra, Makka ni darasa hai la historia ya Uislamu

Kwa mamilioni ya Waislamu, Makka ni kitovu cha ibada—mahali pa kutekeleza Hijja na Umra.

Lakini nyuma ya ibada hizi kuna tabaka jingine la mji huu: historia hai inayosimulia mwanzo wa Uislamu, mapambano yake, na namna ulivyojengeka kuwa dini ya ulimwengu.

Kama anavyoeleza mwandishi Saeed Saeed wa The National, kwa wengi, ziara ya Makka "huenda ikawa ya pekee maishani," hivyo siku za kabla au baada ya ibada huwa fursa muhimu ya kugundua maeneo yenye mizizi ya kina katika historia ya Uislamu .

Moja ya maeneo hayo ni Jabal Al-Nour, maarufu kama "Mlima wa Nuru." Juu yake ndiko lilipo Pango la Hira—mahali ambapo Mtume Muhammad (Allah amnshushie rehema na amani) alipokea wahyi wa kwanza. Safari ya kupanda mlima huo si rahisi; inahitaji subira na nguvu.

Lakini kwa wengi, ugumu huo ni sehemu ya tafakuri, ukikumbusha uzito wa ujumbe ulioshuka hapo. Ni eneo linalochanganya uchovu wa mwili na utulivu wa roho.

Kusini mwa mji kuna Jabal Thawr, ambalo lina Pango la Thawr. Hapa ndipo Mtume na Maswahaba wake Abubakr (Allah amridhie) walijificha kwa siku tatu wakikimbia mateso ya Makafiri wa Quraysh wakati wa Hijra.

Tofauti na Jabal Al-Nour inayohusishwa na mwanzo wa wahyi, Jabal Thawr inasimulia hadithi ya ujasiri, hofu na tawakkul—imani ya kweli kwa Mwenyezi Mungu katika nyakati za hatari.

Karibu zaidi na Msikiti Mkuu kuna Jannat Al-Mualla, makaburi ya kale yanayobeba historia ya watu muhimu katika maisha ya Mtume. Hapa ndipo alipolazwa Khadijah (Allah amridhie), mke wa kwanza wa Mtume na miongoni mwa watu wa mwanzo kabisa kuamini ujumbe wake.

Tofauti na maeneo mengine yenye shughuli nyingi, Jannat Al-Mualla ina ukimya unaolazimisha tafakuri—ikikumbusha kwamba nyuma ya historia kubwa kuna maisha ya watu halisi waliotoa kila kitu kwa ajili ya imani.

Eneo lingine lenye uzito wa kihistoria ni Masjid Al-Bayah. Msikiti huu unahusishwa na ahadi (bay'ah) zilizotolewa na watu wa Madina kabla ya Hijra. Ahadi hizi zilikuwa msingi wa kuanzishwa kwa jamii ya kwanza ya Kiislamu nje ya Makka. Hivyo, Masjid Al-Bayah si jengo tu, bali ni ishara ya mshikamano na ujenzi wa dola ya Kiislamu.

Kwa upande wa kisasa zaidi, Makka pia imeanza kuwasilisha historia yake kupitia taasisi za kielimu kama Makumbusho ya Qur'an. Hapa, wageni wanaweza kufuatilia safari ya Qur'an—kutoka ufunuo wake hadi uhifadhi wake kwa maandishi na usomaji. Ni kiungo kati ya historia ya kale na uelewa wa kisasa wa dini.

Kwa ujumla, maeneo haya yanaifanya Makka kuwa zaidi ya kituo cha ibada. Ni darasa hai linalofundisha historia, imani na uthabiti. Kama Saeed anavyobainisha, yanatoa "mtazamo wa kina zaidi kuhusu mji mtakatifu" —mtazamo unaoweza kubadilisha safari ya ibada kuwa safari ya maarifa na tafakuri.

# KUTOKA KWA MAJIRANI

NA MUGINI SINGIRA



# Mufti wa Uganda azindua kituo cha wakulima Halal

Sheikh Shaban Ramadhan Mubajje amezindua kituo maalum cha wakulima wa Halal nchini Uganda, hatua inayotafsiriwa kama mkakati wa kuimarisha uchumi wa Waislamu kupitia kilimo chenye kuzingatia misingi ya Kiislamu.

Kituo hicho kinalenga kuwajengea wakulima uwezo wa kuzalisha mazao na mifugo inayokidhi viwango vya Halal, sambamba na kuwapatia mafunzo, masoko na uunganisho na sekta ya usindikaji wa bidhaa. Viongozi wa mradi huo wanasema lengo ni kuhakikisha bidhaa za Halal zinapatikana kwa wingi na ubora, huku wakulima wakinufaika kiuchumi.

Uzinduzi huo unaonesha mwelekeo unaokua katika ukanda wa Afrika Mashariki wa kuunganisha dini na maendeleo ya kiuchumi, hasa katika sekta ya chakula. Sekta ya Halal, ambayo inahusisha uzalishaji, usindikaji na usambazaji wa bidhaa zinazoruhusiwa Kiislamu, inatajwa kuwa na fursa kubwa ya ajira na biashara kimataifa.

Hatua ya Uganda inaongeza kasi ya mjadala kuhusu nafasi ya nchi jirani, ikiwemo Tanzania, katika kunufaika na soko hili linalokua kwa kasi duniani. Wataalamu wanaeleza kuwa uwekezaji katika miundombinu ya Halal, elimu kwa wakulima na sera rafiki unaweza kufungua milango ya biashara za ndani na nje ya nchi.

Kwa ujumla, mradi huo unaashiria mabadiliko ya kimkakati—kutoka kilimo cha kawaida kwenda kilimo chenye thamani ya ziada—na kuweka msingi wa uchumi unaojumuisha maadili ya dini na mahitaji ya soko la kisasa.

## Ubalozi wa Kenya waonya ukaguzi mkali Saudi kabla ya Hijja

**RIYADH — Ubalozi wa Kenya nchini Saudi Arabia umetoa tahadhari kwa raia wake kufuata kikamilifu sheria za uhamiaji na ajira, kufuatia hatua za ukaguzi mkali zinazoanza kabla ya msimu wa Hijja.**

**Katika taarifa rasmi, ubalozi huo ulisema mamlaka za Saudi zimeongeza operesheni za ukaguzi zinazolenga wageni wasiokuwa na vibali halali vya ukaazi au wanaofanya kazi nje ya masharti ya visa zao. Hatua hiyo inatarajiwa kuathiri maelfu ya wafanyakazi wa kigeni, wakiwemo Wakenya.**

**Maafisa wameonya kuwa ukiukwaji wa masharti ya visa—ikiwemo kukaa muda uliopitiliza au kubadilisha mwajiri bila ruhusa—unaweza kusababisha faini kubwa, kukamatwa na hata kufukuzwa nchini. Pia kesi za "huroob," ambapo mfanyakazi anatoroka kwa mwajiri wake rasmi, zinapewa kipaumbele katika ukaguzi huo.**

**Wakati huo huo, mamlaka zimeimarisha udhibiti wa kuingia Makka, zikisisitiza kuwa ni mahujaji wenye vibali rasmi vya Hijja pekee watakaoruhusiwa kuingia katika kipindi cha ibada.**

**Onyo hilo linakuja huku Kenya ikitarajia kupeleka takribani mahujaji 5,000 mwaka huu. Viongozi wa Kiislamu wamewataka waumini kufuata taratibu zote za safari na ibada ili kuepuka vikwazo au adhabu za kisheria.**

**Kwa ujumla, hatua za Saudi zinaonyesha msisitizo wa kuimarisha usalama na udhibiti wa umati wakati wa Hijja, huku zikiongeza presha kwa wafanyakazi wa kigeni kuhakikisha nyaraka zao ziko sahihi.**

## HUDUMA ZA KIFEDHA ZA KIISLAMU




UKHTI FATIMA SS

# Nini kitafuata baada ya UAE kujitoa OPEC?

United Arab Emirates imetangaza kujitoa katika kundi la nchi zinazozalisha mafuta (OPEC), hatua inayotajwa kama pigo kubwa kwa kundi hilo la wazalishaji mafuta na ishara ya mabadiliko makubwa katika siasa na uchumi wa nishati duniani.

OPEC iliyoanzishwa mwaka 1960, ikiwa na lengo la kuratibu sera za mafuta za nchi wanachama (ikipanga kiwango cha uzalishaji na udhibiti wa bei) inaundwa hasa Mashariki ya Kati na Afrika.

Uamuzi huo, unaoanza rasmi Mei 1, unaipa UAE uhuru wa kuongeza uzalishaji wa mafuta bila kufungwa na viwango (quotas) vya OPEC, ambavyo kwa miaka mingi vimedhibiti kiasi cha mafuta kinachozalishwa ili kudhibiti bei za kimataifa.




Kwa mujibu wa mamlaka za nishati za UAE, hatua hiyo ni ya kimkakati, ikilenga kuongeza uzalishaji na kukidhi mahitaji makubwa ya nishati duniani.

Kwa muktadha wa kiuchumi, kujitoa huko kunamaanisha UAE inaweza kuongeza uzalishaji hadi zaidi ya mapipa milioni tano kwa siku, ikilinganishwa na kikomo cha chini ilichokuwa imewekewa ndani ya OPEC. Hii inaweza kushusha bei za mafuta kimataifa, hasa wakati ambapo usambazaji umeathiriwa na vita ya Iran na kufungwa kwa Mlango wa Hormuz — njia muhimu inayopitisha takribani asilimia 20 ya mafuta ya dunia.

Hata hivyo, athari zake ni pana zaidi ya soko. Kwanza, hatua hiyo inaonesha mvutano unaokua kati ya UAE na Saudi Arabia, ambayo kwa muda mrefu imekuwa kinara wa OPEC. Pili, inazidisha wasiwasi kuhusu mustakabali wa OPEC yenyewe, huku wachambuzi wakionya kuwa inaweza kupoteza uwezo wake wa kudhibiti bei za mafuta iwapo wanachama wengine watafuata mkondo huo.

Kwa upande wa siasa za kimataifa, uamuzi huu utaifurahisha Marekani ambayo kwa muda mrefu imekuwa ikipinga nguvu ya OPEC katika kupanga bei za mafuta. Pia unaibua uwezekano wa ushindani mkubwa zaidi badala ya ushirikiano katika Ghuba.

# Jukwaa la kimataifa la fedha za Kiislamu kuangazia fursa za Afrika

**ADDIS ABABA — Jukwaa la sita la kimataifa la benki zisizo na riba na takaful linatarajiwa kufanyika Julai 22, 2026 nchini Ethiopia, likilenga kuunganisha wataalamu wa kimataifa na masoko yanayoibukia ya fedha za Kiislamu barani Afrika.**

**Kwa mujibu wa waandaaji, AlHuda CIBE, mkutano huo utabeba kaulimbiu ya "kuunganisha utaalamu wa kimataifa na masoko yanayoibukia ya fedha za Kiislamu Afrika," huku ukilenga kujadili mwelekeo, changamoto na fursa za sekta hiyo inayokua kwa kasi .**

**Taarifa ya waandaaji inaeleza kuwa Afrika ina uwezo mkubwa wa kukuza fedha za Kiislamu kutokana na idadi kubwa ya watu wasiopata huduma za kifedha, pamoja na ongezeko la uhitaji wa mifumo ya kifedha yenye maadili na inayozingatia misingi ya Sharia . Hii inaifanya sekta hiyo kuwa nyenzo muhimu ya kukuza ujumuishaji wa kifedha na maendeleo ya kiuchumi.**

**Katika ajenda, wadau watajadili maeneo muhimu ikiwemo mfumo wa udhibiti (regulation), usimamizi wa Sharia, maendeleo ya takaful, pamoja na nafasi ya teknolojia kama fintech na blockchain katika kupanua huduma za kifedha . Pia, kutakuwa na mjadala kuhusu uwekezaji, ubia kati ya sekta binafsi na serikali, na fursa za biashara za mipakani. Aidha, warsha maalum baada ya mkutano itatoa mafunzo ya vitendo kuhusu usimamizi wa hatari na amana katika benki zisizo na riba, ikiwa ni juhudi za kujenga uwezo wa wataalamu wa sekta hiyo.**

# Indonesia, China kuoanisha viwango vya Halal kabla ya sheria mpya

**JAKARTA — Serikali ya Indonesia imeanza juhudi za kuoanisha viwango vya Halal na China, ikiwa ni maandalizi ya utekelezaji wa sheria ya lazima ya uthibitishaji wa bidhaa za Halal itakayoanza Oktoba 2026.**

**Kupitia Wakala wa Uhakika wa Bidhaa Halal (BPJPH), Indonesia imeanzisha majadiliano na taasisi 18 za Halal kutoka China ili kurahisisha biashara baina ya nchi hizo mbili, huku ikihakikisha ubora na ufuatiliaji wa bidhaa katika mnyororo mzima wa uzalishaji.**

**Mkuu wa BPJPH, Ahmad Haikal Hasan, alisema ushirikiano huo unalenga kuimarisha mfumo mzima wa Halal, ukiwemo ukaguzi, uhifadhi, ufungashaji na usambazaji wa bidhaa. Alieleza kuwa hatua hiyo ni muhimu katika kuhakikisha viwango vinazingatiwa kuanzia uzalishaji hadi sokoni.**

**China imechaguliwa kuwa mshirika wa kwanza kutokana na ukubwa wa soko lake na nafasi yake inayokua katika sekta ya Halal duniani, licha ya kuwa si nchi yenye Waislamu wengi. Indonesia inaamini inaweza kujifunza kutokana na uzoefu wa China katika kusimamia viwango vya Halal katika mazingira ya kimataifa.**

**Hatua hiyo pia inalenga kuongeza mauzo ya nje ya Indonesia na kufanya sekta ya Halal kuwa mhimili wa uchumi wa taifa. Serikali imesema itapanua majadiliano kama hayo kwa nchi nyingine, ikiwemo za Ulaya.**

**Kwa ujumla, mpango huu unaonesha ushindani unaoongezeka kimataifa katika sekta ya Halal, huku nchi zikijipanga kimkakati kunufaika na soko linalokua kwa kasi duniani.**

HUDUMA ZA KIFEDHA ZA KIISLAMU




NA MAHMOUD NYAMGUMA

# Fedha za kiislamu zang'ara katika uchumi wa kijani duniani

Katika hatua inayotafsiri upya mwelekeo wa uchumi wa kimataifa, taasisi ya kifedha Maybank imesisitiza kuwa mfumo wa fedha za Kiislamu unaendana kwa karibu na ajenda za mazingira, jamii na utawala (ESG), huku thamani ya sekta hiyo ikifikia takribani dola trilioni 2.8 duniani.

Afisa Mkuu wa Uendelevu wa Benki hiyo, Datuk Shahril Azuar Jimin, ameripotiwa na tovuti ya Fortune News akisema, misingi ya Kiislamu inayozingatia haki ya kijamii, ustawi wa jamii na kuepuka madhara inaipa nguvu ya kipekee katika kujenga uchumi jumuishi na endelevu.

Kwa mujibu wa World Bank, fedha endelevu katika nchi wanachama wa Ushirikiano wa Kiislamu ziliongezeka kutoka dola bilioni 17.8 mwaka 2017 hadi dola bilioni 82.3 mwaka 2024, ingawa ni asilimia 8.2 tu ya mikopo endelevu iliyokuwa inazingatia sheria za Sharia kati ya 2017 na 2021.

Wataalamu wanaona pengo hili kama fursa kubwa ya kukuza mfumo wa Kiislamu, hasa katika maeneo yanayokabiliwa na changamoto za mabadiliko ya tabianchi kama Kusini Mashariki mwa Asia.

Katika kuonyesha utekelezaji wake kwa vitendo, Maybank kwa kushirikiana na serikali ya Sabah nchini Malaysia ilizindua mpango wa kwanza wa "blue sukuk" duniani, unaolenga kuhifadhi mazingira ya bahari, kuimarisha uvuvi endelevu na kurejesha mifumo ya ikolojia ya pwani.

Hatua hiyo inaendana na mkakati wa taifa hilo wa uchumi wa buluu hadi mwaka 2030, ukilenga sekta kama nishati jadidifu ya baharini, usafirishaji wa kijani na utalii wa kiikolojia.

Hata hivyo, pamoja na mafanikio hayo, changamoto ya pengo la uwekezaji wa kijani bado ipo, ambapo Benki ya Maendeleo ya Asia inakadiria kuwa eneo la ASEAN linahitaji dola bilioni 210 kila mwaka hadi 2030, ilhali lilipokea dola bilioni 27.8 pekee kati ya 2018 na 2019.

Wachambuzi wanaeleza kuwa kuimarika kwa mifumo ya fedha za Kiislamu ikiwemo matumizi ya zana kama zakat na waqf, kunaweza kuwa suluhisho mbadala lenye mizizi ya kimaadili, likichochea maendeleo ya uchumi yanayozingatia haki, usawa na ustawi wa jamii kwa vizazi vijavyo.





# Ujuzi 12 utakaokulipa milele

**Katika mjadala wa mafanikio, hoja moja inazidi kujitokeza kwa nguvu: si kile unachojua pekee kinachokuinua, bali jinsi unavyojihusisha na watu na mazingira yako. Ujuzi laini—soft skills—ndio unaobeba uzito huo.**

**Tofauti na ujuzi wa kitaalamu unaoweza kupitwa na wakati, ujuzi laini hubaki na thamani maisha yote. Ndani ya kazi, biashara, na hata familia, watu wenye ujuzi huu huonekana si tu kama wataalamu, bali kama watu wanaoweza kuaminika, kushirikiana nao, na kuongoza.**

**Msingi wa ujuzi huu huanza na akili ya kihisia. Huu ni uwezo wa kutambua hisia zako na kuzisimamia, huku ukiwa na uelewa wa hisia za wengine. Mtu mwenye akili ya kihisia haogopi mazungumzo magumu; badala yake, huyakabili kwa utulivu na heshima. Anasikiliza kwa makini, anajibu kwa hekima, na anajenga uhusiano wa kuaminiana.**

Baada ya akili ya kihisia, mawasiliano yanafuata kwa umuhimu. Mawasiliano bora si suala la kuzungumza kwa wingi, bali kuwasilisha ujumbe unaoeleweka. Lugha rahisi, sauti tulivu, na uwezo wa kusikiliza hujenga daraja kati ya watu. Kinyume chake, kukatiza wengine au kutumia maneno magumu kupita kiasi huleta mkanganyiko na mara nyingi huzalisha migongano isiyo ya lazima. Mawasiliano ni kiungo kinachounganisha ujuzi mwingine wote.

Lakini hata mawasiliano bora hayawezi kusimama bila nidhamu binafsi. Nidhamu ni uwezo wa kujiongoza bila kusukumwa. Ni kupanga muda, kuweka mipaka, na kudhibiti matamanio ya muda mfupi kwa ajili ya malengo ya muda mrefu. Watu wengi hushindwa si kwa kukosa uwezo, bali kwa kukosa uthabiti wa kufanya yale wanayojua ni sahihi. Nidhamu ndiyo inayogeuza nia kuwa matokeo.

Katika dunia inayobadilika haraka, uwezo wa kubadilika nao unakuwa muhimu. Wale wanaofanikiwa si wale wanaopinga mabadiliko, bali wanaoyakubali na kujifunza kutoka kwayo. Kuwa wazi kwa mawazo mapya, kupokea mrejesho, na kuboresha mbinu ni dalili ya ukuaji. Kukataa mabadiliko au kulaumu mazingira ni njia ya kujizuia mwenyewe kusonga mbele.

Kwa karibu na hilo, kuna tabia ya kuwa mbele ya mambo—proactivity. Hii ni hali ya kuchukua hatua kabla ya kulazimishwa. Ni kuweka malengo binafsi, kutafuta fursa za kuboresha, na kuwajibika kwa matokeo. Watu wanaosubiri maagizo au kulaumu mazingira mara nyingi hubaki nyuma, si kwa sababu hawana uwezo, bali kwa sababu hawachukui hatua.

Ubunifu nao una nafasi yake katika mnyororo huu. Ubunifu si kipaji cha wachache, bali ni uwezo wa kuruhusu fikra huru na kujaribu njia mpya. Mazingira yanayohamasisha mawazo mapya na kukubali makosa kama sehemu ya kujifunza huzaa ubunifu. Hofu ya kushindwa au kushikilia mbinu za zamani huua uwezo huu kabla haujakua.

Wakati huo huo, usimamizi wa muda huamua kama juhudi zote zitazaa matokeo. Muda ni rasilimali isiyoweza kurejeshwa. Kuupangilia vizuri, kuweka vipaumbele, na kuepuka usumbufu huongeza tija. Kuahirisha kazi au kuruhusu vitu visivyo na umuhimu kuchukua nafasi huondoa nguvu ya juhudi zote.

Katika kufanya maamuzi, fikra makini ni nguzo muhimu. Ni uwezo wa kuuliza maswali, kuchambua taarifa, na kupima ushahidi kabla ya kufikia hitimisho. Katika enzi ya taarifa nyingi na mitazamo inayokinzana, mtu asiye na fikra makini huwa rahisi kupotoshwa. Mantiki na uchambuzi vinakuwa kinga dhidi ya maamuzi yasiyo sahihi.

Hakuna mafanikio ya kudumu bila ushirikiano. Uwezo wa kufanya kazi na wengine, kusikiliza, kushirikiana, na kukubali tofauti hujenga nguvu ya pamoja. Watu wanaotawala mazungumzo au kushikilia chuki huathiri timu nzima. Ushirikiano si udhaifu, bali ni nguvu inayozidisha matokeo.

Ndani ya mazingira hayo, uongozi hujitokeza kama matokeo ya tabia, si cheo. Kiongozi bora huongoza kwa mfano, huwahamasisha wengine, na hutoa mrejesho wa kujenga. Anajenga watu badala ya kuwabana. Pale ambapo kuna upendeleo au udhibiti uliopitiliza, imani hupotea na utendaji hushuka.

Katika maingiliano ya kila siku, ujuzi wa kujadiliana huwa muhimu. Ni uwezo wa kufikia suluhisho linalokubalika kwa pande zote. Hii inahitaji utulivu, heshima, na maandalizi. Kufanya mambo kuwa ya kibinafsi au kukimbilia makubaliano huleta hasara badala ya faida.

Mwisho wa yote, ustahimilivu ndio unaobeba ENDujuzi huu wote. Maisha yana changamoto, na si kila juhudi hufaulu mara ya kwanza. Uwezo wa kusimama tena baada ya kushindwa, kujifunza kutokana na makosa, na kuendelea mbele ndiyo unaotofautisha waliofanikiwa na waliokata tamaa. Kukaa kwenye mawazo hasi au kukataa msaada huongeza uzito wa matatizo.

Kwa mtazamo mpana, ujuzi laini si mapambo ya ziada katika maisha ya mtu, bali ni msingi wa mafanikio ya kudumu. Ni uwekezaji wa ndani unaoathiri kila eneo la maisha—kazi, biashara, na mahusiano. Watu wanaoujenga hujikuta wakilipwa si tu kwa fedha, bali kwa heshima, uaminifu, na fursa zisizo na kikomo.

MAHMOUD NYAMGUMA

# Viongozi wa Kiislamu wataka miongozo ya kimaadili ya AI



Katibu Mkuu wa Jumuiya ya Kiislamu DunianI Moahammed Al-Issa, ametoa wito wa kuanzishwa kwa mfumo wa pamoja wa maadili utakaoongoza matumizi ya akili mnemba (AI).

Shirika la Arab News limemnukuu Al-Issa akionya kuwa katika mkutano mkubwa wa kimataifa uliofanyika Fez, Morocco kuwa teknolojia hiyo ikikosa udhibiti inaweza kuchochea chuki, migawanyiko na migogoro ya kijamii.

Mkutano huo uliowakutanisha zaidi ya washiriki 2,000 kutoka nchi 75 ulijadili mustakabali wa ustaarabu wa binadamu katika zama za AI.

Katika hotuba yake, kiongozi huyo alisisitiza kuwa maendeleo ya teknolojia lazima yaongozwe na misingi ya maadili ya pamoja ya kibinadamu, huku ia akibainisha mchango wa wanazuoni wa Kiislamu katika kuweka misingi ya mbinu za kisayansi karne nyingi zilizopita.

Kwa mujibu wa tafiti za kimataifa, sekta ya AI duniani inatarajiwa kufikia thamani ya zaidi ya dola trilioni 15 ifikapo mwaka 2030, hali inayoongeza umuhimu wa kuwepo kwa kanuni thabiti za maadili.

Aidha, Al-Issa alitaka kuwepo uwazi na uwajibikaji zaidi kwa makampuni yanayoendeleza teknolojia hiyo, pamoja na kuweka mipaka madhubuti katika maeneo nyeti kama dini, utamaduni na maamuzi muhimu ya kijamii.

Takwimu za UNESCO zinaonesha kuwa zaidi ya asilimia 60 ya mifumo ya AI iliyopo sasa haina miongozo kamili ya kimaadili, jambo linaloweza kuhatarisha mshikamano wa jamii endapo halitadhibitiwa. Hoja hizo zinaakisi nafasi ya Uislamu kama dira ya maadili katika zama za teknolojia, ikisisitiza kuwa mamlaka ya mwisho lazima yabaki kwa binadamu. Wito huo unaweka msingi wa mjadala mpana kuhusu namna ambavyo maendeleo ya kisasa yanaweza kwenda sambamba na tunu za kiroho na kijamii bila kupoteza utu na mshikamano wa jamii za wanadamu.

# Ukandamizaji waongezeka Jerusalem Mashariki

Mamlaka za Israel zimeendelea na operesheni za msako na kukamata watu katika maeneo ya Jerusalem Mashariki inayokaliwa kwa mabavu, huku walinzi wa Msikiti wa Al-Aqsa wakilengwa moja kwa moja, linaripoti shirika la Anadolu Ajensi la Uturuki.

Hatua hiyo imeibua wasiwasi mpya kuhusu hali ya usalama na uhuru wa ibada kwa Waislamu katika eneo hilo nyeti.

Kwa mujibu wa taarifa hiyo, mlinzi mmoja wa Msikiti wa Al-Aqsa alikamatwa na baadaye kuachiwa kwa masharti magumu ikiwemo kupigwa marufuku kuingia Mji wa Kale kwa siku saba pamoja na kutozwa faini, huku mwingine akifungiwa miezi sita kutokaribia msikiti huo.

Katika kambi ya wakimbizi ya Shuafat, mwananchi mmoja wa Kipalestina alishambuliwa alipokuwa akijaribu kumlinda ndugu yake mwenye ulemavu, ambaye pia alikamatwa kwa muda na kudaiwa kufanyiwa vitendo vya unyanyasaji kabla ya kuachiwa.

Katika eneo la Silwan kusini mwa Al-Aqsa, biashara zilisimamishwa baada ya vikosi vya Israel kuvamia mtaa wa Al-Thawri, kuweka vizuizi na kutoa faini kwa wafanyabiashara na madereva.

Hatua hizi zimetajwa kuwa sehemu ya mkakati mpana unaolenga kudhibiti maisha ya Wapalestina kwa njia ya kiusalama na kiuchumi, hali inayochochea hofu na sintofahamu miongoni mwa wakazi.

Takwimu zinaonesha kuwa takribani walowezi 750,000 wa Israel wanaishi katika Ukingo wa Magharibi, wakiwemo 250,000 katika Jerusalem Mashariki, makazi ambayo yanachukuliwa kuwa kinyume cha sheria za kimataifa. Tangu Oktoba 2023, zaidi ya Wapalestina 1,100 wameuawa na wengine karibu 12,000 kujeruhiwa, hali inayozidisha mjadala wa kimataifa kuhusu haki za binadamu na mustakabali wa amani katika eneo hilo.

MAHMOUD NYAMGUMA

# Mtafiti aonya hali hatari Al-Aqsa, asema udhibiti wa Kiislamu umedhoofika



**AL-QUDS** — Mtafiti wa masuala ya Al-Quds, Dkt. Jamal Amr, ameonya kuhusu kile alichokitaja kuwa hali "hatari na mbaya" inayoikabili Msikiti wa Al-Aqsa, akidai kuwa udhibiti wa Kiislamu katika eneo hilo umefikia kiwango cha kudhoofika kwa kiasi kikubwa.

Akizungumza na Saba News Agency, Dkt. Amr alisema mamlaka za Israel zimechukua udhibiti wa moja kwa moja wa shughuli za msikiti huo, huku usimamizi wa Waqf wa Kiislamu ukibaki kwa jina tu bila nguvu ya utekelezaji.

Alidai kuwa hatua hiyo imeambatana na ongezeko la uvamizi wa walowezi pamoja na kuwekwa kwa ratiba maalum za ibada kwa Wayahudi ndani ya eneo la msikiti, jambo analosema linapingana na makubaliano ya kimataifa na uhuru wa kuabudu.

Kwa mujibu wa ripoti za Kipalestina, maelfu ya walowezi wameingia katika eneo la Al-Aqsa tangu mwanzo wa mwaka huu, huku wengine wakiingia kwa kisingizio cha utalii. Dk. Amr alionya kuwa hali hiyo ni sehemu ya mabadiliko ya kimkakati yanayolenga kubadilisha hadhi ya eneo hilo takatifu.

Aidha, aligusia nafasi ya Jordan katika usimamizi wa maeneo matakatifu, akisema mamlaka yake yamebaki ya kinadharia zaidi kuliko utekelezaji halisi.

Kauli hiyo inaongeza tahadhari juu ya mvutano unaoendelea Mashariki ya Kati, hasa kuhusu mustakabali wa maeneo matakatifu na haki ya Waislamu kuabudu kwa uhuru.

MAHMOUD NYAMGUMA



# Erdogan: Migogoro, mateso ya raia nchi za Waislamu ni huzuni

**ANKARA** — Recep Tayyip Erdoğan amesema ulimwengu wa Kiislamu unapitia kipindi kigumu na cha maumivu, huku akitoa wito wa umoja na mshikamano wakati migogoro ikiendelea katika maeneo kadhaa yenye Waislamu wengi.

Akizungumza katika hafla ya utoaji tuzo ya mashindano ya kimataifa ya usomaji wa Qur'an, kiongozi huyo wa Uturuki alitaja migogoro inayoendelea kuanzia Palestina, Lebanon na Sudan hadi Yemen na Somalia, akisema hali hiyo imejaa huzuni na mateso kwa raia wasiokuwa na hatia.

Erdoğan alikosoa kile alichokiita ukimya wa kimataifa, akidai kuwa jamii inayojitambulisha kama ya "kistaarabu" imekuwa ikifumbia macho mateso yanayowakumba raia, wakiwemo watoto na watu wasio na ulinzi. Aliongeza kuwa baadhi ya mataifa yaliyokuwa yakijinasibu kwa haki za binadamu na usawa sasa yanaonyesha sura tofauti katika nyakati hizi za migogoro.

Katika hotuba yake, alisisitiza umuhimu wa Waislamu kuweka kando migawanyiko ya ndani na kuimarisha mshikamano. Alisema njia pekee ya kuvuka kipindi hicho ni kuaminiana, kushirikiana na kurejea katika misingi ya imani.

Kauli hiyo inakuja wakati mvutano wa kisiasa na kijeshi ukiendelea katika Mashariki ya Kati na maeneo mengine, hali inayozidisha changamoto za kibinadamu katika nchi nyingi za Kiislamu.

# Vita ya Iran yazidi kutikisa mshikamano wa NATO

**BRUSSELS** — Muungano wa kijeshi wa NATO unakabiliwa na mgogoro mkubwa wa ndani unaotishia umoja wake, kufuatia mvutano uliokua hatua kwa hatua kati ya Marekani na washirika wake wa Ulaya, uliotokana na tofauti za muda mrefu za kimtazamo kuhusu usalama wa kimataifa—na hatimaye kulipuka wazi katika vita dhidi ya Iran.

Kihistoria, mvutano kati ya Marekani na Ulaya kuhusu Iran ulianza tangu uamuzi wa Washington kujiondoa katika makubaliano ya nyuklia ya Iran mwaka 2018, hatua iliyopingwa vikali na mataifa ya Ulaya yaliyotaka suluhisho la kidiplomasia. Tofauti hizo zimeendelea kwa miaka, zikijenga msingi wa kutokuaminiana.

Mwaka 2026, mgogoro huo ulifikia hatua mpya baada ya Marekani na Israel kuanzisha mashambulizi dhidi ya Iran bila mashauriano ya kina na washirika wa NATO. Mataifa mengi ya Ulaya yalikataa kushiriki katika operesheni hizo, yakisisitiza kuwa vita hivyo si sehemu ya majukumu ya NATO na havikuwa na makubaliano ya pamoja.

Mvutano ulizidi pale Washington ilipoomba msaada wa kijeshi ili kulinda usafirishaji wa mafuta katika Mlango wa Hormuz, lakini nchi nyingi za Ulaya zikakataa, zikisema wazi: "Hii si vita yetu" . Hatua hiyo ilichochea kauli kali kutoka kwa Rais Donald Trump, aliyekosoa wazi washirika wake na kuhoji thamani ya muungano huo.

Katika mazingira hayo ya kutofautiana, ndipo hatua kama kupunguza wanajeshi nchini Ujerumani zilipoibuka— ikiwa ni matokeo ya mgawanyiko uliokwishajengeka.

Katika uamuzi uliotangazwa wiki hii, Trump ameamua kupunguza wanajeshi wa Marekani barani Ulaya, ikiwa ni pamoja na mpango wa kuondoa wanajeshi takribani 5,000 nchini Ujerumani, hatua iliyozua wasiwasi ndani ya jumuiya hiyo huku viongozi wakionya kuwa hatua hiyo inaweza kudhoofisha uwezo wa muungano huo wa kujilinda na kuzuia vitisho.

Hata ndani ya Marekani, baadhi ya wabunge wameonya kuwa hatua hizo zinaweza kudhoofisha uwezo wa NATO kuzuia vitisho.

Waziri Mkuu wa Poland, Donald Tusk, alieleza uzito wa hali hiyo akisema: "Tishio kubwa kwa jumuiya ya NATO si maadui wa nje, bali ni kusambaratika kwa muungano wetu."

Kwa sasa, NATO inakabiliwa na swali la msingi: je, ni muungano wa ulinzi wa pamoja wa Ulaya, au chombo cha kufanikisha ajenda pana za usalama za Marekani? Tofauti ya majibu ya swali hilo ndiyo mzizi wa mgogoro wa sasa.

Iwapo tofauti hizi hazitatatuliwa, wachambuzi wanaonya kuwa muungano huo unaweza kuendelea kudhoofika, huku Ulaya ikianza kujitegemea zaidi kijeshi—hatua inayoweza kubadilisha kabisa mizani ya nguvu ndani ya NATO na mfumo mzima wa usalama wa kimataifa.

Msamvu, Morogoro
P.O.Box 6011
Morogoro,
Tanzania

Mhariri
+255 789 201383

# Tutafakari upya matumizi ya viboko shuleni

Aprili 30 kila mwaka, Tanzania huungana na nchi nyingine duniani kuadhimisha Siku ya Kimataifa ya Kukomesha Adhabu za Viboko, ikiwa ni sehemu ya jitihada za kuhamasisha malezi bora na mbinu mbadala za nidhamu zisizohusisha ukatili kwa wanafunzi.

Katika maadhimisho ya kitaifa mwaka huu yaliyofanyika jijini Dar es Salaam, wadau mbalimbali, mashirika ya haki za watoto, na asasi za kiraia wametoa wito kwa Serikali kuboresha mifumo ya kisheria na kanuni ili kukomesha adhabu ya viboko na aina nyingine za ukatili unaotweza utu wa watoto.

Wadau hao wamesema adhabu za viboko bado ni miongoni mwa aina za ukatili zinazokubalika kijamii na zinaendelea kuwaathiri watoto katika shule, madrasa na nyumbani.

Kutokana na hali hiyo, wameishauri Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia kupanua matumizi ya nidhamu chanya kitaifa kupitia sera zilizo wazi, mafunzo ya kina kwa walimu na ufuatiliaji endelevu.

Aidha, walimu wameshauriwa kuunda mazingira salama na jumuishi darasani yanayoheshimu utu wa mtoto kwa kuzingatia Waraka wa Elimu Na. 24 wa mwaka 2002 unaohamasisha nidhamu isiyo ya ukatili.

Wamesema kuwa licha ya Tanzania kusaini mikataba mbalimbali ya kupinga adhabu ya viboko, vitendo hivyo bado vinaendelea na ni miongoni mwa aina za ukatili dhidi ya watoto. Suala la adhabu ya viboko shuleni linaendelea kuibua mjadala mzito nchini, baadhi ya watu wakitaka iendelee kutumika na wengine wakitaka iachwe.

Sisi, gazeti la Imaan tunasema, kutoa adhabu ni njia mojawapo ya kupambana na maadili mabaya katika jamii, na ni jambo kongwe la enzi na enzi lililoelezwa katika vitabu vyote vya dini kuanzia Taurati, Zaburi, Injili na hatimaye Qur'an Tukufu.

Katika Biblia, ambayo chimbuko lake ni mafundisho ya Injili ya Nabii Isa (amani ya Mwenyezi Mungu imshuke), kuna andiko lisemalo: "Usimnyime mtoto wako mapigo maana ukimpiga kwa fimbo hatakufa. Utampiga kwa fimbo na kuokoa nafsi yake na kuzimu." [Taz: Kitabu cha Mithali 13–14].



Katika Uislamu, adhabu ya viboko imetajwa kama njia ya kuwaadabisha watenda maovu ya uzinifu, n.k. Mwenyezi Mungu anasema: "Mzinifu mwanamke na mzinifu mwanaume wachapeni mijeledi mia moja kila mmoja wao..." [Qur'an 24:2].

Kwa upande wa watoto, Mtume wa Mwenyezi Mungu (rehema za Allah na amani imshukie) amesema: "Waamrisheni watoto kusali wakifikisha miaka saba na wachapeni viboko (wakiacha au kupuuza sala) wakiwa na miaka 10." [Ahmad na Abu Daudi].

Kwa hiyo, suala la watoto kuchapwa viboko, kwa mujibu wa mafundisho ya dini zote za mbinguni halina mjadala. Kinachoangaliwa ni kiasi cha hivyo viboko ambacho katika Uislamu kimeelezwa kuwa ni kipigo kisichoacha alama mwilini.

Tafiti pia zinaonesha kuwa mataifa jirani yenye tamaduni zinazofanana na Tanzania, kama Kenya, Uganda na Sudan Kusini, baadhi yamefanikiwa kutumia mbadala wa adhabu ya viboko unaofanya kazi vizuri.

Hivyo, inawezekana kwa walimu kurekebisha tabia za wanafunzi bila kutumia adhabu kandamizi na mwanafunzi akabadilika. Inasikitisha kuona wanafunzi wakiacha shule kwa kukimbia viboko, huku wengine wakipata majeraha makubwa, ulemavu au hata kupoteza maisha kutokana na adhabu hiyo.

Ushauri wetu kwa walimu watumie mbinu mbadala za malezi, zikiwamo kumpa mwanafunzi zawadi za kushtukiza (surprise) au kitu anachokipenda, pamoja na kujenga urafiki naye.

SHEIKH
Shaaban Mussa
0786 272 323

# Dhikr, uhai wa moyo baada ya Ramadhan

Miongoni mwa neema kubwa ambazo Muislamu alizipata ndani ya mwezi wa Ramadhan ni kulainika kwa moyo wake na kuongezeka kwa hamasa ya kumkumbuka Mwenyezi Mungu (dhikr).

Ndani ya mwezi huo mtukufu, ndimi zetu zilizoea kutamka Tasbih, Tahmid, Takbir na Istighfar. Nyoyo zikawa karibu zaidi na Mola wao, na nafsi zikapata utulivu wa kipekee. Hii inaonesha wazi kwamba Ramadhan si mwezi wa kufunga tu, bali ni msimu wa kuhuisha moyo kwa dhikr. Hata hivyo, swali la msingi linabaki: je, hali hii tunaidumisha hata baada ya Ramadhan kuisha?

Dhikr ni kumtaja Mwenyezi Mungu kwa ulimi na moyo, kwa namna tulizofundishwa. Inajumuisha kauli kama "Subhanallah", "Alhamdulillah", "Allahu Akbar", "Astaghfirullah", pamoja na dua na usomaji wa Qur'an.

Dhikr ina nafasi kubwa mno katika maisha ya Muislamu. Ni chanzo cha utulivu wa moyo, kama Mwenyezi Mungu Anavyosema: "Wale walioamini na nyoyo zao zikatulia kwa kumkumbuka Mwenyezi Mungu. Hakika, kwa kumkumbuka Mwenyezi Mungu nyoyo hutulia." [Qur'an, 13: 28].

Aya hii inaweka wazi kwamba utulivu wa kweli haupatikani kwa mali, umaarufu au mafanikio ya dunia, bali hupatikana kwa dhikr. Kadri Muislamu anavyozidi kumkumbuka Mwenyezi Mungu, ndivyo moyo wake unavyozidi kuwa na amani.

Vilevile, Mtume (Allah amshushie rehema na amani) amesema: "Mfano wa anayemkumbuka Mola wake na asiyemkumbuka ni kama aliye hai na mfu." [Bukhari].

Hii inaonesha wazi kwamba dhikr ni uhai wa moyo; kuiacha ni kuukaribisha umauti wa kiroho. Ndani ya Ramadhan, mazingira yalikuwa rahisi kwa kufanya dhikr kwa wingi. Baada ya swala, wakati wa kufunga na kufuturu, na katika usiku tuliojaaliwa, ndimi hazikukaa bila kumtaja Mwenyezi Mungu.


Lakini baada ya Ramadhan, wengi hurudi katika hali ya kupunguza dhikr au kuisahau kabisa. Hii ni hatari kwani moyo usiomkumbuka Mwenyezi Mungu huwa dhaifu na rahisi kushawishika na maovu.

Muislamu anapaswa kuelewa kuwa dhikr si ibada ya msimu, bali ni pumzi ya maisha ya kiroho. Kama mwili unavyohitaji chakula, ndivyo moyo unavyohitaji dhikr ili uendelee kuwa hai.

Miongoni mwa njia za kudumisha dhikr ni kujiwekea ratiba ya kila siku: adhkari za asubuhi na jioni, Tasbih baada ya swala, na Istighfar kwa wingi. Aidha, nyakati zisizo na shughuli nyingi—kama kutembea, kusubiri au kusafiri—zinaweza kutumika kufanya dhikri na kujaza muda kwa kheri.

Ni muhimu pia kufanya dhikr kwa moyo uliohudhuria, si kwa ulimi peke yake. Dhikr yenye athari ni ile inayotoka katika moyo unaotafakari.

Moja ya faida kubwa ya dhikr ni kwamba humkinga Muislamu dhidi ya wasiwasi na huzuni. Mwenyezi Mungu Anasema: "Na anayejiepusha na kumkumbuka Mimi, basi hakika atapata maisha yenye dhiki..." [Qur'an, 20: 124]. Hii inaonesha kuwa kuacha dhikr huleta dhiki ya ndani, hata kama mtu anaonekana kuwa na kila kitu cha dunia.



Na hapa ndipo wanazuoni wametoa onyo kali. Amesema Ibn Qayyim al-Jawziyya: "Kwa hakika wingi wa kumkumbuka Mwenyezi Mungu ni kinga dhidi ya unafiki, kwani wanafiki humkumbuka Mwenyezi Mungu kidogo. Mwenyezi Mungu Amesema: '...Wala hawamkumbuki Mwenyezi Mungu isipokuwa kidogo.'" [Qur'an, 4:142].

Kauli hii inaonesha kwamba kupunguza dhikri si jambo dogo; linaweza kuwa dalili ya ugonjwa wa moyo. Kadiri dhikr inavyopungua, ndivyo hatari ya kupotea kiroho inavyoongezeka.

Aidha, dhikr huimarisha uhusiano wa mja na Mola wake. Kadiri mtu anavyozidi kumkumbuka Mwenyezi Mungu, ndivyo anavyohisi ukaribu na rehema Zake. Ni muhimu pia kujifunza adhkari sahihi kutoka katika mafundisho ya Mtume, ili dhikr iwe sahihi na yenye tija zaidi.

Kwa hakika, moyo ulio hai ni ule unaomkumbuka Mwenyezi Mungu. Na moyo uliokufa ni ule uliosahau dhikr. Hivyo basi, baada ya Ramadhan, kila mmoja wetu ajiulize: je, ulimi wangu bado unamtaja Mwenyezi Mungu kama ulivyokuwa ndani ya Ramadhan? Je, moyo wangu bado unapata utulivu kwa dhikr?

Pamoja na hilo, kuna jambo jingine muhimu linalothibitisha uimara wa imani ya Muislamu: msimamo thabiti (Istiqamah) katika njia ya haki.

Katika makala inayofuata, tutazungumzia kuhusu Istiqamah – Kusimama imara baada ya Ramadhan, na jinsi ya kubaki katika njia sahihi bila kuyumba baada ya mwezi mtukufu kuondoka.

ذوالقعدة فتاوى



SHEIKH
Shaaban Mussa
0786 272 323

# Yaruhusiwa kufupisha swala nyuma ya imamu mkazi?

**Swali: Ikiwa msafiri atawakuta wakazi katika rakaa mbili za mwisho akiwa nyuma ya imamu mkazi, je, atatoa salamu pamoja naye kwa nia ya kufupisha (swala)?**

**Jibu:** Haijuzu kwa msafiri, ikiwa anaswali nyuma ya mkazi, kufupisha swala, kwa ujumla wa kauli ya Mtume (Allah amshushie rehema na amani): "Mlichokikuta kiswalini, na kilichowapita kikamilisheni."

Kwa hiyo, ikiwa msafiri atawakuta wakazi wapo katika rakaa mbili za mwisho akiwa pamoja na imamu mkazi, ni lazima aswali rakaa mbili nyingine baada ya imamu wake kutoa salamu, na haijuzu kutoa salamu pamoja na imamu kwa kujitosheleza na rakaa mbili tu. Na Allah ndiye Mjuzi zaidi.

**Swali: Je, inajuzu kwa mtu kuswali swala ya faradhi nyuma ya mtu anayeswali sunna?**

**Jibu:** Kauli sahihi ni kwamba haitadhuru kutofautiana kwa nia kati ya imamu na maamuma. Na inajuzu kwa mtu anayeswali faradhi kuswali nyuma ya mtu anayeswali sunna.

Kama alivyokuwa Muadh ibn Jabal akifanya hivyo katika zama za Mtume Muhammad (Allah amshushie rehema na amani), ambapo alikuwa akiswali pamoja na Mtume swala ya Isha, kisha anarudi kwa watu wake na kuwaswalisha swala hiyo hiyo; kwake ilikuwa ni sunna, lakini kwao ilikuwa ni faradhi.

Kwa hiyo, mtu akiingia msikitini wakati wewe unaswali faradhi au sunna, kisha akasimama mtu pamoja nawe ili mswali kwa jamaa, basi hakuna ubaya. Swala yenu ni sahihi. Ataingia pamoja nawe na ataswali kile atakachokikuta, na baada ya kumaliza kwako, Yeye atasimama kukamilisha alichobakiza ikiwa alipitwa na kitu, iwe ulikuwa unaswali sunna au faradhi. Na Allah ndiye Mjuzi zaidi.

**Swali: Je, ni katika Sunna mtu kuswali rakaa mbili kabla ya Magharibi baada ya adhana?**

**Jibu:** Ndiyo, ni katika Sunna kuswali rakaa mbili kabla ya swala ya Magharibi, yaani kati ya adhana na iqama.

Mtume (Allah amshushie rehema na amani) aliamrisha hilo mara tatu, akasema: "Swalini kabla ya Magharibi, swalini kabla ya Magharibi, swalini kabla ya Magharibi," lakini katika mara ya tatu akasema: "Kwa anayetaka," ili watu wasilichukulie kuwa ni Sunna ya lazima (ratiba ya kudumu).

Hivyo, kuswali rakaa mbili kabla ya Magharibi (kati ya adhana na iqama) ni Sunna, lakini si Sunna ya kudumu (ratiba), kwa hiyo si vyema kudumu nayo kila wakati; kwa sababu mtu akidumu nayo itakuwa kama Sunna ya kudumu. Tofauti na rakaa mbili baada ya Magharibi, hizo ni Sunna ya kudumu inayopendekezwa kuizingatia, isipokuwa katika safari.

Ama msafiri, haisuniwi kwake kuswali Sunna za kudumu za Adhuhuri, Magharibi, au Isha. Na Mtume (Allah amshushie rehema na amani) amesema: "Kati ya kila adhana mbili (yaani adhana na iqama) kuna swala," yaani kuna swala ya hiari (nafila). Lakini kwa swala ya Alfajiri na Adhuhuri, hizo zina Sunna za kudumu, wakati wa Alasiri, Magharibi, na Isha si za kudumu. Na Allah ndiye Mjuzi zaidi.

ذُو القِعدة

**NASAHA ZA WIKI**
**0787 503 085**



NA YUSUFU AMINI



# Uislamu ni matendo mema, tenga muda kuyafanya

Mara nyingi nimekuwa nikieleza kwamba Uislamu si dini ya kufikirika, bali ni dini ya kimatendo na njia sahihi ya maisha inayoweza kumrudishia mwanadamu heshima na utu wake.

Kwa maana hiyo, Uislamu si dini ya maneno matupu wala ibada za nje pekee; ni mfumo kamili wa maisha uliojengwa juu ya matendo mema yanayoakisi maadili ya Kiislamu.

Mtu anayedai kuwa imani yake kwa Allah ni kubwa lakini hajishughulishi na ibada, imani yake hiyo haimsaidii hapa duniani wala mbele ya Allah Ta'ala Siku ya Kiyama. Muislamu anatakiwa kuonesha imani yake kupitia vitendo vinavyomnufaisha yeye binafsi na jamii inayomzunguka.

Thamani ya Uislamu huonekana katika matendo mema, si katika kauli pekee. Qur'an Tukufu imeunganisha mara nyingi imani na matendo mema, ikisisitiza kuwa mambo hayo hayawezi kutenganishwa.

Allah anaeleza kuwa walioamini na wakatenda mema watapata ujira mkubwa, jambo linaloonesha kuwa imani ya kweli lazima idhihirike kwa vitendo vinavyoleta manufaa, huruma na haki.

Katika maisha ya kila siku, matendo mema si lazima yawe makubwa au ya gharama kubwa. Tabasamu kwa nduguyo, kumsaidia mwenye uhitaji, kumzuru mgonjwa, au hata kuondoa kikwazo njiani ni miongoni mwa matendo yanayopendeza mno mbele ya Allah.

Mtume (Allah amshushie rehema na amani) amesisitiza kuwa tendo dogo linaweza kuwa na uzito mkubwa mbele ya Allah ikiwa litafanywa kwa nia njema. Hata hivyo, changamoto kwa wengi ni kudhani hawana muda wa kufanya matendo mema.

Ukweli ni kwamba matendo mema hayahitaji muda mwingi, bali moyo wa kujali na utayari wa kuyafanya. Kutenga muda kwa ajili ya ibada kama sala, dhikr na kusoma Qur'an ni msingi muhimu wa kumjenga Muislamu kiroho.

Vilevile, kuwasaidia wengine ni sehemu ya ibada, kwani Uislamu unafundisha uwiano kati ya haki za Allah na haki za viumbe wake. Ni muhimu pia kutambua kuwa matendo mema yana athari si tu kwa mhusika bali kwa jamii nzima.

Jamii yenye watu wanaojaliana, kusaidiana na kuheshimiana huwa na amani, mshikamano na maendeleo. Kinyume chake, kukosekana kwa matendo mema hupelekea chuki, ubinafsi na migogoro. Aidha, kutenda mema ni njia ya kuimarisha nafsi, kuijenga jamii, kupata radhi za Allah na kufutiwa madhambi.

Katika ulimwengu wa sasa wenye pilika nyingi ni rahisi kusahau wajibu huu muhimu. Ndiyo maana kuna haja ya kutenga muda wa kufanya matendo mema mara kwa mara.

Ratiba ndogo tu inaweza kuleta mabadiliko makubwa katika maisha binafsi na kwa wale wanaokuzunguka. Kwa mfano, unaweza kutoa sadaka kila Ijumaa, kuwazuru wagonjwa mara moja kwa wiki au kushiriki kusafisha msikiti.

Ibada ndogo kama hizi zinaweza kuwa na athari kubwa na kuleta baraka nyingi kwenye maisha yako.

## Ikhlas katika ibada

Hata hivyo, matendo mema yanapaswa kufanywa kwa Ikhlas na unyenyekevu, si kwa ajili ya kusifiwa au kuonekana mbele za watu. Nia njema ndiyo inayobadili tendo la kawaida kuwa ibada yenye thamani kubwa.

Ni hasara iliyoje kwa mtu kufanya juhudi katika ibada kisha akose thawabu kutokana na kukosekana kwa Ikhlas. Allah anasema: "Ambaye ameumba mauti na uhai ili kukujaribuni ni nani miongoni mwenu mwenye vitendo vizuri zaidi. Na yeye (Allah) ni Mwenye nguvu Mwenye Msamaha." [Qur'an, 67:2]. Akifafanua aya hii, Al–Fudhail bin Iyaadh amesema: "Kauli ya Allah 'Mwenye vitendo vizuri zaidi' ina maana ya amali iliyotendwa kwa Ikhlas na usahihi. Hivyo amali yoyote itakapokuwa na Ikhlas lakini isiwe sahihi Allah haikubali.

Kwa hiyo, ni wajibu kutakasa nia na kuchunga moyo, kwani Allah Mtukufu anasema katika hadithil Qudsiy: "Mimi ni Mkwasi, simuhitajii yeyote katika ushirika wangu. Atakayefanya amali akanishirikisha na kitu kingine, basi nitaikataa (amali hiyo) pamoja na mshirika wake (yaani, mtu hatopata ujira wowote kwa amali hiyo)." [Muslim na Ibn Majah].

Aidha, Mtume (Allah amshushie rehema na amani) amesema: "Hakika Allah hatazami viwiliwili vyenu wala sura zenu, bali anatazama nyoyo zenu." [Muslim].

ذوالقعدة

MAKALA MAALUM



SHEIKH
Seif Ruga
0712 690 811

# Malezi ya yatima na usimamizi wa mali yake

**Sharia ya Kiislamu imeweka mkazo mkubwa katika kulinda haki za mayatima, hususan katika usimamizi wa mali zao. Waislamu wameamrishwa kuwalea mayatima, kuwatunza, kuwajenga katika maadili mema ya dini na kuwalinda dhidi ya aina yoyote ya uonevu au unyanyasaji – hasa katika mali zao.**

**Kula au kutumia mali ya yatima kinyume cha sharia ni miongoni mwa madhambi makubwa yaliyotajwa wazi katika Qur'an Tukufu. Kutoka kwa Sahl bin Sa'ad (Allah amridhie) ameeleza kuwa Mtume (rehema na amani zimshukie) amesema: "Mimi na yule anayemlea yatima (kwa wema) tutakuwa hivi Peponi...," akaashiria kidole chake cha kati na cha shahada.**

Katika Uislamu, yatima amepewa haki zote muhimu kama ilivyo kwa mtoto mwingine yeyote. Hata hivyo, pamoja na kuwepo kwa mikataba ya kimataifa inayozungumzia haki za watoto, bado kuna upungufu katika kueleza kwa uwazi haki mahsusi za mayatima.

Kwa mfano, Tamko la Geneva la mwaka 1924, Kifungu cha Pili kinasisitiza wajibu wa kuwahifadhi na kuwaokoa mayatima, lakini halitoi mwongozo wa kina kuhusu malezi ya kiroho na maadili kama inavyoelekezwa na Uislamu.

Vivyo hivyo, Tamko la Haki za Mtoto la mwaka 1959 halijaainisha kwa uwazi haki za mayatima, bali linatoa miongozo ya jumla inayoweza kufasiriwa bila kutaja upekee wao. Kwa zaidi ya karne 14, sharia ya Kiislamu imekuwa mstari wa mbele katika kubainisha na kulinda haki za yatima.

Mfano ni uwepo wa hukumu ya kulipa fidia (ghurra) kwa mtoto aliye tumboni endapo mama yake atathibitika kumdhuru na kusababisha kifo chake. Hii inaonesha jinsi Uislamu unavyolinda haki za mtoto tangu akiwa tumboni.

## Yatima ni nani?

Wanazuoni wa sharia ya Kiislamu (Fuqahau) wameeleza kuwa yatima ni mtoto aliyefiwa na baba yake kabla ya kufikia umri wa balehe. Kwa ufafanuzi zaidi, wanazuoni wamewagawa mayatima katika makundi mawili; yatima halisi na yatima wa kihukumu.

Yatima halisi ni mtoto aliyefiwa na baba yake kabla ya kufikia balehe, hata kama mama yake bado yu hai. Kwa upande mwingine, yatima wa kihukumu ni mtoto ambaye baba yake yupo hai, lakini hali yake inafanana na ya yatima halisi kutokana na kukosa malezi au msaada kutoka kwa baba yake.

Hali hii inaweza kujitokeza pale baba anapotoweka, hajulikani alipo, amemtelekeza mtoto, au hana uwezo wa kumlea kutokana na umasikini, maradhi makubwa au kifungo cha muda mrefu. Katika mazingira hayo, mtoto huyo hupewa hukumu ya yatima ili alindwe na kupewa haki zake kikamilifu.

Uislamu unahimiza kuwafanyia wema mayatima, kuwalea kwa upendo na kulinda mali zao kwa uadilifu hadi watakapofikia balehe na kuwa na uwezo wa kusimamia mali zao.

Allah anasema: "Na wapeni mayatima mali zao, wala msiwabadilishie kizuri kwa kibaya, wala msile mali zao kwa kuziunganisha na mali zenu. Hakika kufanya hivyo ni dhambi kubwa." [Qur'an, 4:2]. Mlezi anaruhusiwa kutumia mali ya yatima kwa manufaa ya yatima mwenyewe, kama vile uwekezaji au kukidhi mahitaji yake.

Hata hivyo, mlezi akiwa tajiri hapaswi kuchukua chochote katika mali hiyo; na akiwa masikini anaweza kutumia kiasi kidogo kwa haki na bila kufuja. Allah anasema: "Na aliyekuwa tajiri ajizuilie (kuchukua ujira), na aliye fakiri ale kwa kadri ya ada (kiasi kinachokubalika)..." [Qur'an, 4:6].

Baadhi ya wanazuoni, akiwamo Abu Al–Aaliya wanaeleza kuwa mlezi anapopata uwezo anapaswa kurejesha alichokichukua kutoka katika mali ya yatima.

## Aina mbili za malezi ya yatima

Malezi ya yatima yapo aina mbili. Kwanza ni kumlea na kumtunza nyumbani pamoja na familia hadi atakapobalehe, na pili ni kumpatia msaada wa kifedha au mahitaji muhimu ikiwa anaishi nje ya familia.

Ingawa kuishi naye nyumbani kunasisitizwa zaidi, kutoa msaada kwa yatima anayeishi mahali pengine nako kuna thawabu kubwa. Wanazuoni wamekubaliana kuwa mlezi au msimamizi wa mali ya yatima anaruhusiwa kuwekeza au kufanya biashara kwa kutumia mali hiyo ili izalishe.

Hata hivyo, kuna tofauti ya maoni kuhusu iwapo mlezi anaweza kuchukua sehemu ya faida ya biashara hiyo kama ujira wa juhudi zake. Madhehebu ya Hanafi na baadhi ya wanazuoni wa Hanbali wameruhusu hilo, lakini wanazuoni wa Malik na Shafi wamekataza.

Hoja ya wanaokataza ni kwamba, faida itokanayo na biashara hiyo ni mali ya yatima hivyo haiwezi kuchukuliwa bila mkataba sahihi, na mlezi hawezi kujifanyia mkataba binafsi wa biashara (Al–Mudharaba). Hata hivyo, kauli ya kuruhusu inaonekana kuwa na nguvu zaidi, kwa sharti la kuepuka upendeleo au kujinufaisha kupita kiasi.

MAKALA MAALUM

SEHEMU YA 2

Na Said Rajab
0783 650 803

# Kwanini Ulaya wamekataa kushirikiana na Trump?

**Katika sehemu ya kwanza ya makala haya wiki iliyopita, tulijadili kwa kifupi dhamira na malengo ya mashambulizi ya uchokozi ya Marekani dhidi ya Iran, ambapo tuliona jinsi Marekani ilivyokumbana na upinzani mkali usiotarajiwa.**

**Iran ilijibu kwa haraka na kwa nguvu ikitumia makombora ya balistiki na hypersonic kuharibu vituo kadhaa vya kijeshi vya Marekani katika eneo la Mashariki ya Kati. Pia iliishambulia kwa nguvu Israel, mshirika mkuu wa Marekani na kusababisha uharibifu mkubwa.**

**Katika sehemu hii ya pili na ya mwisho, tunajibu swali la kwa nini Ulaya imekataa kushiriki katika vita hiyo.**



Ulaya, pamoja na China na Urusi zinaelewa wazi kuwa mafanikio ya Marekani katika kuidhibiti Mashariki ya Kati yangeiweka Ulaya chini ya ushawishi wake kwa muda mrefu. Hali hiyo imezifanya nchi hizo kutafuta kujinasua kutoka katika ushirika usio na tija, ambao kwa mtazamo wao haujaleta manufaa bali hasara.

Ulaya iliidhinisha mkataba wa NATO unaosisitiza ulinzi wa pamoja pale mwanachama anaposhambuliwa, lakini kifungu hicho hakijatumika katika mashambulizi ya uchokozi yaliyoanzishwa na Marekani na Israel dhidi ya Iran.

Vilevile, ripoti za kijasusi kutoka baadhi ya nchi za Ulaya zimeeleza kuwa Iran haikuwa tishio la moja kwa moja linalohitaji hatua ya vita kamili.

Msuguano umeongezwa pia na hatua ya Marekani, chini ya uongozi wa Donald Trump kuwaacha washirika wake wa Ulaya kubeba mzigo mkubwa wa mgogoro wa Ukraine.

Kwa upande mwingine, Marekani imetuhumiwa kunufaika na mvurugiko wa usambazaji wa gesi ya Urusi katika masoko ya Ulaya – hali ambayo kwa kiasi fulani ilichangia kuibuka kwa fursa ya kuuza gesi yake kwa bei ya juu zaidi.

Matokeo yake, kumeshuhudiwa kuibuka kwa ushirikiano usio rasmi kati ya baadhi ya mataifa ya Ulaya, Urusi na China, wenye lengo la kupunguza ushawishi wa Marekani katika siasa za kimataifa.

Ushirikiano huo hauchochewi na uungwaji mkono wa moja kwa moja kwa Iran, bali unatokana na nia ya kuilazimisha Marekani kubeba gharama na athari za maamuzi yake yenyewe.

Hata hivyo, kuna uhalisia mgumu wa kisiasa na kijiografia. Nchi hizi hazitamani kuona Marekani ikidhoofika kupita kiasi au kushindwa kabisa, kwa kuwa hali hiyo inaweza kuacha ombwe kubwa la kiusalama katika Mashariki ya Kati – eneo ambalo hakuna taifa lenye uwezo wa kulidhibiti kwa haraka.

Hofu kubwa kwa mataifa ya Ulaya ni kwamba, kushindwa kwa Marekani kunaweza kuisukuma kujitenga ndani ya mipaka yake na kuiacha dunia, hususan Mashariki ya Kati katika hali ya machafuko na utawala wa nguvu pekee (law of the jungle), yaani mwenye nguvu kumla mnyonge.

Katika mazingira hayo, hali inaweza kuwa mbaya zaidi kabla ya kupatikana kwa mfumo mbadala wa kudumisha utulivu wa kimataifa, hasa kwa kuzingatia nafasi ambayo Marekani imekuwa ikicheza kama 'polisi wa dunia'.

Kwa msingi huo, Ulaya inatamani kuwa na Marekani ambayo ni mshirika wa kweli, siyo dola yenye hulka ya kulazimisha matakwa yake. Wanahitaji ushirikiano unaozingatia maslahi ya pamoja, badala ya mfumo unaoonekana kunufaisha upande mmoja kwa gharama ya wengine.

Ustahimilivu wa Iran pamoja na kupungua kwa hadhi ya Marekani katika macho ya dunia umeibua mjadala mpya kuhusu mizania ya nguvu za kimataifa. Hoja inayojitokeza ni kwamba, nguvu iliyodhaniwa kuwa haiwezi kushindika inaweza kudhoofishwa pale kunapokuwa na mshikamano na maamuzi ya pamoja ya mataifa ya Waislamu.

TUJIFUNZE
AI (ARTIFICIAL INTELLIGENCE)

Na Junaynat Ally Dama

# AI inavyoharibu sanaa ya uandishi kwa wanafunzi




Katika miaka ya hivi karibuni, akili bandia (Artificial Intelligence – AI) imeingia kwa kasi katika mazingira ya elimu, hasa katika uandishi wa kitaaluma. Wanafunzi wengi sasa hutegemea zana hizi kuandika insha, kufanya uchambuzi, na hata kujenga hoja. Kwa juu juu, hali hii inaonekana kama maendeleo ya kiteknolojia yanayorahisisha kazi. Lakini kwa mtazamo wa kitaaluma, kuna mjadala mzito unaoibuka: je, AI inasaidia uandishi au inaudhoofisha?

Profesa Wendy Laura Belcher anaeleza wazi kuwa athari za AI kwa uandishi wa wanafunzi si ndogo. Anatahadharisha kwamba tunakaribia kuzalisha kizazi kisichoweza kuandika—na kwa maana pana, kisichoweza kufikiri. Kauli hii si ya kubahatisha; inatokana na uchunguzi wa moja kwa moja wa maandishi ya wanafunzi yanayotumia AI.

Tatizo la kwanza ni kwamba AI huzalisha hoja zilizo wazi kupita kiasi (banal arguments). Badala ya uchambuzi wa kina, maandishi yanajaa mawazo ya kawaida yasiyo na ubunifu. Kwa kuwa AI hutabiri maneno yanayotarajiwa zaidi, matokeo yake huwa ni mawazo yale yale yanayojirudia—bila upekee wala kina. Hii inaondoa kabisa kiini cha uandishi wa kitaaluma, ambao unahitaji kufikiria nje ya yaliyo dhahiri.

Pili, maandishi ya AI huwa marefu lakini matupu. Sentensi zinaweza kuwa sahihi kisarufi na kuvutia kisauti, lakini hazina maana ya kina. Profesa Belcher anaonyesha kuwa AI huunganisha maneno maarufu ili kuunda sentensi "nzuri," lakini ambazo hazitoi mchango wowote wa kifikra. Hii ni hatari kwa mwanafunzi anayefikiri kuwa urefu wa maandishi ni sawa na ubora wake.

Tatizo jingine ni kukosekana kwa muunganiko wa mawazo. AI hubadilisha istilahi na majina mara kwa mara ili kuepuka kurudia, lakini matokeo yake ni kupotea kwa mstari mkuu wa hoja. Msomaji hulazimika kujitahidi kufuatilia mada, kwani hakuna uthabiti wa istilahi. Hapa, kile kinachoitwa ubunifu wa lugha kinageuka kuwa kikwazo cha uelewa.

Aidha, AI hutumia misamiati ya kitaaluma vibaya. Inaweza kujaza sentensi kwa maneno mazito kama "metaphor" au "complexity," lakini bila maana halisi. Matokeo yake ni maandishi yanayoonekana ya kitaaluma, lakini yasiyoeleweka. Hii ni kama kujenga nyumba nzuri kwa nje lakini isiyo na msingi imara.

Kuhusu uhusiano wa hoja, AI mara nyingi huchanganya sababu na matokeo. Hutumia maneno kama "inaonyesha" au "inasisitiza" bila kueleza wazi nini kinaathiri nini. Hii husababisha upotoshaji wa mantiki, jambo ambalo ni hatari katika uandishi wa kitaaluma unaotegemea ushahidi.

Zaidi ya hayo, AI huondoa nafasi ya mwandishi kama mfasiri wa maandishi. Badala ya mwanafunzi kuonekana kama anayechambua, maandishi huonekana kana kwamba "maandishi yenyewe" ndiyo yanazungumza. Profesa Belcher anaonya kuwa hali hii inawafanya wanafunzi wajione hawana nafasi katika uandishi wao wenyewe.

Tatizo lingine ni matumizi kupita kiasi ya vivumishi vya sifa. AI hupamba sentensi kwa maneno mengi ya tathmini, lakini mara nyingi hayalingani na maana halisi. Sentensi zinaweza kusikika vizuri, lakini zinapochunguzwa kwa kina, zinakuwa hazina mantiki.

Kwa upande mwingine, AI inaweza kuingiza upendeleo wa kijamii au hata ubaguzi bila mwanafunzi kutambua. Profesa Belcher anaonyesha kuwa baadhi ya maandishi ya AI yanaelekea kuhukumu tamaduni zisizo za Magharibi kwa viwango vya Magharibi. Hii ni hatari kwa wanafunzi ambao hawajafundishwa kuchambua mitazamo hiyo kwa kina.


Pia kuna tatizo la wizi wa hoja (plagiarism). AI inaweza kuchukua mawazo yaliyopo tayari na kuyawasilisha kama mapya. Mwanafunzi asiye makini anaweza kuwasilisha kazi isiyo yake bila kujua. Hii si tu ukiukwaji wa maadili, bali pia inaua ubunifu wa mwanafunzi.

Hatimaye, AI mara nyingi hukosea hata katika mambo ya msingi. Inaweza kutoa taarifa zisizo sahihi kuhusu vitabu, waandishi, au historia. Hii inaonyesha wazi kuwa AI si chanzo cha uhakika cha maarifa, bali ni chombo kinachohitaji uangalifu mkubwa.

Kwa jumla, hoja ya Profesa Belcher ni wazi: uandishi ni mchakato wa kufikiri. Pale ambapo mwanafunzi anapokabidhi jukumu hilo kwa

MUSSA IMANI SHEHA ZANZIBAR
0773 181 494

SEHEMU YA 6



# SIMULIZI YA MTUME MUSA (AMANI YA ALLAH IMSHUKIE)

## VISA VYA MITUME NA MASWAHABA

**Makala yetu katika wiki iliyopita ilitufikisha pale Mtume Musa (amani ya Allah imshukie) alipofunga mkataba wa ajira ya miaka nane kama mahari ya binti wa bwana mkubwa mmoja huko Madyana, na akawa kama mmoja kati ya wanafamilia ya mzee huyo.**

**Nabii Musa alikazia mkataba ule kwa kusema: "Hili ni baina yangu na wewe, muda wowote kati ya miwili nikiumaliza kusiwe na uadui (hiyana) juu yangu, na Allah ni shahidi juu ya tuyasemayo [Qur'an, 28:28)**

### Utumishi na maandalizi

Musa (Amani ya Allah imshukie) aliitumikia ajira yake kwa uaminifu mkubwa, uadilifu na kwa moyo mkunjufu. Hiki kilikuwa ni kipindi kingine muhimu cha kujiandaa na kazi nzito inayomkabili ya utume baada ya kile kipindi cha kuishi karibu na watawala wa serikali ya Fir-aun Misr.

Kipindi hiki, kadhalika, kipindi cha maandalizi ya kuipokea kazi ngumu ya kuwaongoza watu wakaidi katika njia ya haki. Kilikuwa ni kipindi muhimu cha kujipanga kuupokea utume uliojaa hoja dhidi ya watawala majabari zimuwezeshe kuwakomboa wanyonge na kuipindua serikali ya wahuni.

### Mitume wote kupitia kazi ya ufugaji

Kwa mujibu wa hadith ya Mtume Muhammad (Allah amshushie rehema na amani), iliyosimuliwa na Abu Huraira, kila Mtume alipitia kazi ya kuchunga kondoo na mbuzi. Mtume alipoulizwa: "Na wewe pia uliwahi kufuga? Alijibu: "Ndio, nilikuwa nikiwafugia wakuu wa Makka kwa pesa ndogo waliyokuwa wakinilipa." [Ibn Majah].

Inaelezwa kuwa, hekima yake ni kujifunza tabia ya subira, upole na busara katika kuwaongoza watu.

### Musa arejea Misr

"Basi Musa alipotimiza muda, akasafiri pamoja na ahali zake (kurejea kwao Misri) aliona moto upande wa mlimani akawaambia ahli (jamaa) zake, 'Ngojeni hakika nimeona moto labda nitakuleteeni habari za huko au kijinga cha moto ili muote.'" [Qur'an, 28:29].

Moto ulikuwa ni kielelezo cha wito wa Allah kumuita mja wake Musa kumpa Utume rasmi. "Basi alipoufikia aliitwa kutoka upande wa kuliani mwa bonde, katika kiwanja kilichobarikiwa, kutoka mtini, 'Ewe Musa, njoo mbele na usiogope, kwa yakini wewe ni miongoni mwa waliosalimika'" [Qur'an, 28:30].

Katika pahala pengine inaelezwa: " Na je zimeshakufikia habari za Musa? Alipouona moto akawaambia watu wake, 'Ngojeni, nimeuona moto, huenda nikakuleteeni kijinga katika huo moto, au nitapata muongozo katika huo moto (wa kuniongoza njia).'"

Basi alipoufikia akaitwa: "Ewe Musa, bila shaka Mimi ndiye Mola wako, basi vua viatu vyako, hakika wewe uko katika Bonde Takatifu la Tuwa. Na mimi nimekuteua (kuwa Mtume) basi yasikilize unayoletewa (yanayofunuliwa kwako)."

"Kwa yakini Mimi ndiye Mwenyezi Mungu, hakuna aabudiwae kwa haki ila Mimi, basi niabudu na usimamishe swala kwa kunitaja. Bila shaka kiama kitakuja nataka kusudi kukificha (nisiseme lini kitafika) ili kila nafsi ilipwe kwa yale iliyoyafanya. Basi wasikuzuie na (kuyaamini) hayo wale wasiokiamini wafuatao matamanio, usije ukaangamia." [Qur'an, 20:9-17].

### Maelezo

Hivi ni kusema kwamba kuanzia hapo, Musa (amani ya Allah imshukie), aliupokea rasmi utume. Katika hatua za awali alitakiwa kujua kwamba yuko katika mahali patakatifu, ambapo haifai kukanyaga kwa viatu, basi avuwe.

Pili, aliimarishwa kiimani kwa kupatiwa misingi mikuu ya mafunzo ya Kiislamu ambayo Mitume wote walipewa na kuwafikishia watu wao, nayo ni kuamini uwepo wa Allah Muumba ambaye pekee anastahiki kuabudiwa, kuamini akhera, (hesabu na malipo kwa mujibu wa matendo ya mja).

Vilevile, Mtume Musa (amani ya Allah imshukie), katika bonde lile takatifu aliagizwa kutekeleza swala kama ibada kuu ya kumtaja na kumkumbuka Mwenyezi Mungu. Lakini jambo jengine kubwa, alitakiwa kuwa na tahadhari na wasioamini akhera, wanaoongozwa na utashi wa nafsi zao, wasije kumpotosha.

### Nabii Musa apewa miujiza

Kila Mtume hupewa miujiza kama kielelezo cha ukweli wa madai yake kwamba yeye ni Mtume wa Allah. Kwa mfano, Mtume Ibrahim alitupwa motoni akatoka bila ya kuathirika, Mtume Swaleh alitolewa ngamia jike jabalini, Mtume Muhammad mwezi ulipasuka na kuwa vipande viwili baada ya Makureish kumuomba hilo nk. Basi, kadhalika, Mtume Musa naye alipewa miujiza kadhaa. Baadhi ya miujiza hiyo alipewa siku ileile na akiwa mahala palepale alipopewa utume, nayo ni fimbo yake kugeuka nyoka na mkono wake kuwa mweupe sana hautizamiki baada ya kuutoa kwapani!

Qur'an inasema: "Na ni nini hicho kilichomo mkononi mwako?' (Musa) akasema, 'Hii ni fimbo yangu, naiegemea na ninainamishia majani kwa ajili ya wanyama wangu, tena ninaitumia kwa matumizi mengine.' Mwenyezi Mungu akasema, 'Itupe (chini) ewe Musa', akaitupa, mara ikawa nyoka anayekwenda (anayetembea).

Na Junaynat Ally Dama

# Mitazamo 10 potofu kuhusu unene

Mjadala kuhusu unene umejaa kauli rahisi zinazosikika kama ukweli—lakini nyingi ni potofu. Tatizo si tu kutoelewa, bali athari zake: unyanyapaa, sera dhaifu, na huduma zisizo rafiki kwa wagonjwa.

Makala ya Sarah Hutter, ikiripoti utafiti wa University of Connecticut Rudd Center for Food Policy and Health inaeleza kuwa mitazamo hasi kuhusu uzito mara nyingi hujificha katika maamuzi ya kila siku—kuanzia jinsi watu wanavyotathminiwa kazini hadi namna wanavyohudumiwa katika mfumo wa afya—hata bila wahusika kutambua.

## Dhana potofu: Unene si ugonjwa

Ukweli: Unene unatambuliwa rasmi kama ugonjwa sugu unaojirudia. Shirika la Afya Duniani (WHO) linaeleza kuwa unatokana na mwingiliano wa maumbile, biolojia ya ubongo, tabia za kula, na mazingira. Hii ina maana kuwa si jambo la "kupenda kula" pekee. Kuutazama kama ugonjwa kunasaidia mifumo ya afya kufuatilia tatizo, kutenga rasilimali, na kutoa matibabu stahiki.

## Dhana potofu: Uzito mkubwa ni sawa na afya mbaya

Ukweli: Uzito peke yake hauamui afya. Wapo watu wenye uzito mkubwa lakini wana viashiria vizuri vya kiafya—sukari, shinikizo la damu, na cholesterol viko sawa. Vivyo hivyo, mtu mwenye uzito mdogo anaweza kuwa na tabia hatarishi (lishe duni, kutofanya mazoezi). Hivyo, tathmini ya afya inahitaji kuangalia picha nzima, si namba ya uzito pekee.

## Dhana potofu: Unene ni "uchaguzi wa maisha"

Ukweli: Kauli hii ni rahisi, lakini si sahihi. Tafiti zinaonyesha kuwa biolojia ya mwili huathiri njaa, kushiba, na jinsi kalori zinavyotumika. Mazingira ya chakula (upatikanaji wa vyakula vya bei nafuu vilivyosindikwa, matangazo, ratiba za kazi) nayo yana mchango mkubwa. Ripoti ya The Lancet Global Health iliyotajwa katika makala hiyo inaonya kuwa simulizi la "ni chaguo lako" huendeleza unyanyapaa na kuchelewesha hatua za sera.

## Dhana potofu: Aibu na shinikizo vinawasaidia watu kupunguza uzito

Ukweli: Kinyume chake ndicho hutokea. Unyanyapaa wa uzito (weight stigma) huongeza msongo wa mawazo, unaoweza kusababisha kula kupita kiasi na kujitenga kijamii. Utafiti unaonyesha uhusiano na ongezeko la wasiwasi, msongo wa mawazo, na hata kujidhuru. Hivyo, aibu si "motisha"—ni kikwazo.

## Dhana potofu: Tatizo ni la nchi zilizoendelea tu

Ukweli: Unene unaongezeka duniani kote. Tangu 1990, viwango vimepanda kwa kasi katika nchi nyingi, zikiwemo zinazoendelea. Mabadiliko ya mfumo wa chakula, miji, na mtindo wa maisha yamefanya tatizo hili kuwa la kimataifa. Hata inawezekana nchi zinazoendelea zinaathirika zaidi kwa sababu ya ulaji mwingi wa wanga.

## Dhana potofu: Lishe na mazoezi pekee vinatosha—na vinadumu

Ukweli: Lishe na mazoezi ni muhimu, lakini si suluhisho la peke yake kwa wengi. Biolojia ya mwili hufanya upunguzaji wa uzito kuwa mgumu kudumisha. Tafiti zinaonyesha watu wengi hurudisha sehemu kubwa ya uzito waliopunguza ndani ya miaka michache. Hii inaonyesha hitaji la mbinu jumuishi—ikiwemo ushauri wa kitaalamu, mabadiliko ya mazingira, na wakati mwingine matibabu.

## Dhana potofu: Wataalamu wa afya hawana unyanyapaa

Ukweli: Unyanyapaa dhidi ya wenye uzito upo hata katika huduma za afya ambapo baadhi ya wahudumu hupunguza muda au juhudi wanazotoa kwa wagonjwa hao. Hili linaweza kuathiri uchunguzi, mawasiliano, na matokeo ya matibabu. Suluhisho ni mafunzo ya kitaaluma na mifumo inayopunguza upendeleo.

## Dhana potofu: Ubaguzi wa uzito si tatizo kubwa

Ukweli: Kijamii, ubaguzi wa uzito mara nyingi hukubalika kuliko aina nyingine za ubaguzi. Kisheria, ulinzi wake ni mdogo katika maeneo mengi. Hii inaathiri ajira, elimu, na huduma za afya. Kutambua uzito kama eneo la haki za kijamii ni hatua muhimu ya marekebisho.

## Dhana potofu: Vichekesho vya uzito ni "mzaha tu"

Ukweli: Vichekesho hivi huendeleza mitazamo hasi na vina athari za kisaikolojia kwa muda mrefu. Watafiti wanavilinganisha na aina nyingine za vichekesho vya kibaguzi—vinaweza kuonekana vidogo, lakini hujenga mazingira ya kudhalilisha.

## Dhana potofu: Sekta ya chakula haina mchango

Ukweli: Mazingira ya chakula yana nafasi kubwa. Upatikanaji wa vyakula vilivyosindikwa, bei nafuu ya kalori zisizo na lishe, na matangazo makubwa huunda uchaguzi wa watu. Watafiti wanakiri kuwa ni vigumu kutenganisha mchango wa kila kipengele, lakini mazingira haya yanaonekana kuwa dereva mkuu wa ongezeko la unene.

ذو القعدة

## MATUKIO YENYE MAZINGATIO

NA ZAHARANI BARAKA

# Umuhimu wa mahujaji kuwaiga Salaf

**Ibrahim bin Yazid (Allah amrehemu) amesema, Yusuf bin Mahak alisimulia kuwa Umar bin Khattwab alitoka nyumbani akaona msafara wa watu, akauliza: "Ni wasafiri gani hawa?" Wakaambiwa: "Ni mahujaji." Umar akauliza mara tatu: "Je, kuna jambo jingine lililowatoa (kwao) zaidi ya Hijja?" Wakajibu: "Hapana." Umar akasema: "Lau wasafiri hawa wangejua wamefikia kwa nani, basi macho yao yangetulia kwa furaha ya fadhila baada ya msamaha. Naapa kwa Yule ambaye nafsi ya Umar iko mkononi mwake, ngamia yoyote hakunyanyua kwato zake wala kuziweka chini isipokuwa Allah amemnyanyua daraja moja mtu aliyempanda ngamia huyo, amemfutia dhambi moja, na kumwandikia jema moja."' *[Muswannaf Abdulrazaq]*."**

### Mafundisho ya tukio

Wema waliopita (Salaf) ni miongoni mwa viumbe bora zaidi hapa ulimwenguni baada ya Mitume na Manabii wa Allah (amani ya Allah iwashukie).

Hawa ni pamoja na Masahaba wa Mtume (Allah awaridhie wote), waliowafuata kwa wema, na wale waliofuata njia yao katika elimu, adabu, tabia njema, uelewa wa dini na kufuata mwenendo wa Mtume (rehema na amani zimshukie).

Mtume amesema: "Watu bora zaidi ni wa karne yangu, kisha wanaowafuatia, kisha wanaowafuata." [Bukhari na Muslim]. Hadith hii inaonesha ubora wao kwa ujumla; si lazima kila mmoja awe bora kuliko watu wa baada yao, bali wao ndiyo watu bora zaidi katika umma huu.

Miongoni mwao wamo waliobashiriwa Pepo wakiwa pamoja na Mtume (rehema na amani zimshukie). Kwa mantiki hiyo, waja wema ndiyo walioifahamu Qur'an na Sunna kwa usahihi, na wao ndiyo wa kuigwa katika dini.

### Ufahamu wao kuhusu Hijja

Salaf walielewa vyema maana ya Hijja, lengo lake, hekima yake na madhumuni yake. Walikuwa na nguvu katika ibada, unyenyekevu na ukweli katika kujikurubisha kwa Allah, wakitekeleza ibada hii kwa nyoyo safi.

Aidha, walisisitiza ulazima wa kutekeleza Hijja mapema na walipendelea kuhiji mara kwa mara. Baadhi yao, akiwamo Taus bin Kaysan, Sa'id bin Al–Musayyib na wengine wengi walihiji zaidi ya mara arobaini.

### Ikhlas katika Hijja

Salaf walijali sana kutakasa nia zao, na hawakuhiji kwa lengo la kujionesha (ria), kusifiwa, majivuno wala kutafuta umaarufu wa kuitwa Al–haji. Umar (Allah amridhie) aliwaonya kwa kusema: "Mnakuwa na nywele zilizochafuka, mavumbi na jasho, na hamkusudii chochote cha dunia, ilhali hatujui safari nyingine iliyo bora kuliko hii."

Ibn Umar alipoambiwa kuwa mahujaji ni wengi alisema: "Hapana! Wengi wao ni wasafiri, na mahujaji wa kweli ni wachache." Yaani, wengi huenda Makka lakini wanaohiji kwa Ikhlas ni wachache.

Baadhi ya Waislamu huenda Hijja kwa maslahi binafsi; wengine huifanya Hijja kama ziara ya kitalii, wakizurura na kupiga picha katika maeneo ya kihistoria badala ya kujibidiisha na ibada.

Ikhlas ni kipengele muhimu katika Hijja na ibada nyinginezo. Hivyo, Muislamu anatakiwa kuitumia vyema ibada hii. Ikumbukwe kuwa Hijja bora iliyotekelezwa kwa ukamilifu malipo yake ni Pepo.

Malipo haya hayapatikani kwa mzaha; anayapata yule anayefahamu thamani ya ibada hii na akaitekeleza kwa umakini mkubwa huku akiomba taufiki ya Allah katika kila hatua.

### Safari ya Hijja

Wema waliopita walisaidiana wakati wa safari za Hijja na walitoa mali zao kwa ajili ya wengine. Mujahid amesema: "Nilisafiri na Ibn Umar katika Hijja, naye alikuwa akinisaidia."

Kadhalika, Abdullah bin Mubarak alikuwa akikusanya pesa za wenzake wakati wa safari, anawahudumia njiani, kisha analipa matumizi yote; na baada ya kurejea nyumbani anawapa tena pesa zao.

### Ibada zao msimu wa Hijja

Waja wema walipovaa Ihram (mavazi maalum ya Hijja) walikuwa wakitetemeka kwa hofu ya kutokubaliwa ibada yao ya Hijja.

Ali bin Al–Husayn alipokusudia kusoma Talbiyah, uso wake ulibadilika rangi na kutetemeka, akisema: "Nahofia nisije kukataliwa." Naye Anas bin Malik (Allah amridhie) alipohirimia Hijja alikuwa hazungumzi mambo ya dunia hadi amalize ibada hiyo.

Katika siku ya Arafa, waja wema walimwomba Allah msamaha, walilia sana na kusali kwa unyenyekevu wakihofia dua zao kutokubaliwa. Ali bin Abi Twalib (Allah amridhie) amesema: "Hakuna siku ambayo Allah anawaacha huru watu wengi kutokana na Moto kuliko siku ya Arafa." [Muslim].

Sufyan Ath–Thawri alipoulizwa ni nani mwenye hali mbaya zaidi katika mkusanyiko wa Hijja alijibu: "Ni yule anayefikiri kwamba Allah hatawasamehe watu hawa."

Tofauti iliyopo kati yetu na wema waliotangulia ni kwamba, wao walikuwa makini zaidi na dini, walijua hakika ya dunia, walimcha Allah zaidi na walifuata Sunna kwa usahihi zaidi. Hivyo, anayetaka kufikia daraja yao anatakiwa kufuata njia yao na kumuabudu Allah kwa usahihi kama walivyofanya wao.

Miongoni mwetu wapo wanaokwenda Hijja kwa nia ya kutembea tu, wengine wakikusudia kufanya biashara, na baadhi wakivutiwa na safari. Wapo pia wanaolenga kupata umaarufu kwa kuitwa Al–haji au Hajjat.

ذُوالقِعدَة

MAKALA MALEZI

JUNAYNAT ALLY DAMA



# Namna ya kuzungumza na watoto kuhusu mitandao ya kijamii

Katika enzi ya kidijitali, mitandao ya kijamii si tena chaguo—ni sehemu ya maisha ya watoto. Simu janja na intaneti zimefungua dunia ya taarifa, mawasiliano, na burudani. Lakini pamoja na fursa hizo, kuna hatari zinazogusa afya ya akili, maadili, na usalama. Hivyo, jukumu la mzazi si kuzuia tu, bali kuongoza kupitia mazungumzo yenye maana.

Ukweli wa msingi ni huu: njia bora ya kupunguza hatari za mtandaoni si udhibiti mkali, bali uhusiano imara. Mtoto anapomwamini mzazi, huwa tayari kushirikisha yale anayokutana nayo. Hapo ndipo malezi ya kidijitali huanza—sio kwa sheria, bali kwa mawasiliano ya wazi.

Mazungumzo haya yanapaswa kuanza mapema. Watoto wengi huanza kutumia majukwaa mapya kabla hata wazazi hawajayafahamu. Kusubiri tatizo litokee ni kuchelewa. Mazungumzo ya mapema hujenga mazingira ambapo mtoto anaweza kusema ukweli bila hofu. Hii ni kinga bora kuliko adhabu ya baadaye.

Changamoto kwa wazazi wengi si umuhimu wa mazungumzo, bali namna ya kuanza. Suluhisho ni rahisi lakini la kimkakati: badili mtazamo. Anza kwa udadisi, si hukumu. Muulize mtoto akuonyeshe majukwaa anayopenda na kwa nini anayatumia. Mpe nafasi awe "mwalimu." Njia hii humfanya ajisikie kuthaminiwa, na hukupa uelewa wa moja kwa moja wa dunia yake.

Mazungumzo yanapokuwa ya vitendo zaidi, yanafanikiwa zaidi. Kaa na mtoto anapotumia mtandao. Tazama video anazopenda, uliza kuhusu watu anaowafuata, au mambo yanayomvutia. Angalia pia mapendekezo ya algorithimu—yanatoa picha ya kile kinachomzunguka kisaikolojia. Hapa, mzazi haingilii, bali anaelewa.

Maswali ya wazi ni zana muhimu. Badala ya kuuliza "unatumia muda mwingi mtandaoni?" uliza "unapenda nini kuhusu jukwaa hili?" au "unajisikiaje watu wanapopenda unachoweka?" Maswali haya yanachochea fikra na mazungumzo ya kina. Lengo si kupata majibu ya haraka, bali kuelewa uzoefu wa mtoto.

Ni muhimu pia kwa mzazi kushiriki maarifa yake kwa busara. Badala ya kutoa onyo la moja kwa moja, tumia mifano ya matukio halisi—kama ulaghai mtandaoni au changamoto hatarishi—kuanzisha mjadala. Hii hupunguza ulinzi wa mtoto na humfanya awe tayari kushiriki.

Hata hivyo, mafanikio ya mazungumzo haya hutegemea majibu ya mzazi. Mtoto akisema jambo linalotia wasiwasi, hasira au hukumu huweza kufunga mawasiliano. Utulivu, kusikiliza, na kuthibitisha uelewa hujenga usalama wa kihisia. Mtoto anahitaji kujua kuwa anaweza kusema bila kuadhibiwa.

Katika hatua hii, elimu ya hatari inapaswa kuwa ya wazi lakini yenye mizani. Watoto wanapaswa kuelewa masuala ya faragha, udumu wa taarifa, na hatari ya kuwasiliana na watu wasiojulikana. Unyanyasaji wa mtandaoni, uvujaji wa taarifa, na maudhui yasiyofaa ni changamoto halisi. Lakini elimu hii haipaswi kuogopesha—ipaswa kuwawezesha.

Wakati huo huo, ni kosa kuiona mitandao ya kijamii kama tishio pekee. Inaweza kuimarisha mahusiano, kukuza ubunifu, na kuwapa watoto nafasi ya kujieleza. Inaweza kuwasaidia kupata jamii ya watu wanaofanana nao au kujifunza mambo mapya. Lengo la mzazi si kuikataza, bali kuisimamia kwa uwiano.

Changamoto kubwa zaidi iko kwenye athari za kisaikolojia. Watoto wanapojilinganisha na maisha ya mtandaoni, wanaweza kujiona hawatoshi. Hapa ndipo mzazi anapaswa kuingilia kwa hekima—kuwasaidia kutofautisha kati ya uhalisia na taswira inayopambwa. Mtoto anapaswa kuelewa kuwa kile kinachoonekana mtandaoni si picha kamili ya maisha.

Hatua nyingine muhimu ni kuweka mipaka kwa makubaliano. Badala ya amri, tengeneza kanuni za familia kuhusu matumizi ya mitandao: muda wa kutumia, mahali pa kutumia, na aina ya maudhui yanayokubalika. Hii hujenga uwajibikaji badala ya uasi.

Kwa ujumla, mazungumzo haya si tukio la mara moja, bali ni mchakato unaoendelea. Kadri mtoto anavyokua, ndivyo mazungumzo yanavyobadilika. Kila mtoto ni tofauti—kwa umri, tabia, na mazingira—hivyo hakuna mwongozo mmoja unaofaa wote.

MAKALA
SAIKOLOJIA

UKHTI FATIMA SS




# Kwa nini mijadala mikutanoni haifikii hitimisho lenye tija?

Ni jambo la kawaida leo kusikia malalamiko ya watu waliotoka kwenye mkutano wakisema, "tumejadili sana, lakini hakuna kilichobadilika." Kwa nje, mijadala mingi huonekana kuwa yenye tija—watu wanachangia, mawazo yanatolewa, na muda unatumiwa kikamilifu. Lakini kwa undani, hakuna maamuzi thabiti, hakuna mwelekeo mpya, na hakuna hatua zinazofuata. Swali la msingi linabaki: tatizo liko wapi?

Uchambuzi wa kitaalamu unaonyesha kuwa tatizo si mikutano yenyewe, bali ni namna mijadala inavyoendeshwa. Watu wengi huingia kwenye mjadala wakiwa na lengo la "kushinda hoja" badala ya kutatua tatizo. Hii hubadilisha kabisa mwelekeo wa mazungumzo. Badala ya kujenga suluhisho la pamoja, kila mshiriki hujikita katika kulinda msimamo wake. Matokeo yake, mijadala hubaki katika mzunguko usio na mwisho.

Moja ya sababu kuu ni kuepuka hoja halisi (avoidance). Mara nyingi, masuala muhimu hayazungumzwi moja kwa moja. Kauli kama "tutaangalia hilo baadaye" au "hilo ni nyeti kidogo" hutumiwa kufunika matatizo halisi. Hii si kwa sababu watu hawajui tatizo, bali kwa sababu wanaamini kulizungumzia hakutaleta mabadiliko au kutaibua mgogoro. Matokeo yake ni mikutano inayozunguka juu juu ya tatizo bila kuligusa kiini chake.

Sababu ya pili ni utamaduni wa kulaumiana (blame). Badala ya kuuliza nini kimeharibika katika mfumo, mijadala hujikita katika nani amekosea. Maswali kama "nani alifanya makosa?" au "nani hakutekeleza?" hutawala. Hii inaweza kuonekana kama uwajibikaji, lakini kwa hakika huua mjadala wa kweli. Watu wanapohisi wanahukumiwa, wanajilinda badala ya kushirikiana. Hivyo, tatizo halitatuliwi—linahamishwa tu kutoka mtu mmoja kwenda mwingine.

Sababu ya tatu, ambayo mara nyingi haionekani wazi, ni groupthink. Hapa, watu huonekana kukubaliana, lakini si kwa sababu wanaamini kile kinachosemwa, bali kwa sababu hawataki kupingana na wengine. Katika mazingira ya "kuwa wema" au "kuwa team player," watu huchagua kukaa kimya hata wanapokuwa na maoni tofauti. Kwa nje, mkutano unaonekana kuwa na umoja; kwa ndani, hakuna makubaliano ya kweli.

Mchanganyiko wa mambo haya matatu huunda kile kinachoweza kuitwa "mzunguko wa mijadala isiyo na tija." Kadri watu wanavyoepuka ukweli, kulaumiana, au kukubaliana kimya kimya, ndivyo mijadala inavyozidi kukwama. Na kadri inavyokwama, ndivyo watu wanavyopoteza imani kwamba mijadala inaweza kuleta mabadiliko. Hapo ndipo mikutano inaanza kuwa formaliti tu—si chombo cha maamuzi.

Kuna pia tatizo la mwelekeo wa muda. Mijadala mingi hukwama kwa sababu inalenga sana yaliyopita badala ya yajayo. Watu wanatumia muda mwingi kuchambua makosa ya nyuma badala ya kujadili nini kifanyike sasa. Hii huongeza mzigo wa lawama na kupunguza uwezekano wa suluhisho.

Suluhisho, kwa mujibu wa wachambuzi wa mawasiliano ya kikundi, ni kubadili aina ya mazungumzo—kutoka "mjadal a wa kushindana" kwenda "mjadal a wa kusonga mbele." Hii inamaanisha mambo mawili kwa wakati mmoja: kwanza, kushughulikia tatizo halisi bila kulikwepa; pili, kuelekeza mjadala kwenye suluhisho la baadaye badala ya makosa ya zamani.

Kwa vitendo, hii inahitaji mabadiliko ya kimfumo. Viongozi wanapaswa kuunda mazingira ambayo watu wanaweza kusema ukweli bila hofu. Pia, mijadala inapaswa kuongozwa na maswali sahihi—si "nani amekosea?" bali "tubadilishe nini ili kosa lisijirudie?" Zaidi ya hayo, ni muhimu kuwa na nafasi ya makusudi ya kupinga hoja (devil's advocate) ili kuvunja ukimya wa groupthink.

Kwa kifupi, mijadala haikosi hitimisho kwa sababu watu hawana akili au mawazo, bali kwa sababu ya mifumo ya mawasiliano inayowazuia kutumia uwezo wao kikamilifu. Pale ambapo mijadala inakuwa ya kweli, inayolenga tatizo halisi na kuangalia mbele, ndipo mikutano hubadilika kutoka kuwa mazungumzo yasiyo na mwisho hadi kuwa chombo cha maamuzi yenye tija.